# Nipashe

Jumamosi Mei 23, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580239

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Wabunge wengine waikimbia Chadema wakiibua shutuma

UKURASA 4




UKURASA 11

# ACT yatoa msimamo Membe kuwania urais

UKURASA 2



Bernard Membe

## BAA LA CORONA



Kama una uwezo wa kutoka na kutembea au kuendesha baiskeli kwa ajili ya mazoezi, kumbuka kunawa mikono kwa maji na sabuni kabla ya kutoka nyumbani, unaporudi mazoezini kama hakuna maji karibu, unaweza kutumia kimiminika chochote chenye pombe kupaka mikono yako. WHO

* **Epuka mikusanyiko ya watu**
* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

# Ripoti ya CAG moto bungeni



**BUNGE** lataka vigogo kibao washughulikiwe

UKURASA 3

## TAREHE MTIHANI KIDATO 6 YATAJWA

UKURASA 2


Scan Hapa

**MICHEZO** LIGI KUU BARA BILA MASHABIKI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# ACT yatoa msimamo Membe

**Na Enock Charles**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimebainisha msimamo kuhusu uwezekano wa kumpa nafasi ya kuwa mgombea wake wa urais, aliyekuwa kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Benard Membe.

Katika mahojiano maalum na Nipashe jijini Dar es Salaam mwanzoni mwa wiki, Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, alisema ikitokea kada huyo akajiunga na chama hicho na kutimiza vigezo vinavyotakiwa, anaweza kupewa nafasi hiyo.

Alisema ACT-Wazalendo inatambua kile alichokiita kutotendewa haki kwa baadhi ya wanachama wa chama tawala, CCM wakati wa mchakato wa uchaguzi mkuu.

"Tuna imani kwamba baadhi ya watu watataka 'kum-challenge' (kuchuana na) Rais John Magufuli, kwa mfano tumemsikia ndugu Membe ambaye amefukuzwa uanachama. Lakini, kwa taarifa zilizopo ni kwamba anaendelea kutetea uanachama wake.

"Sasa kwa mfano akigombea, 'I am trying to build a scenario' (ninajaribu kutengeneza hoja) na akashindwa harakati hizo ndani ya CCM, akija ACT kugombea hatuwezi kumzuia, mradi akitimiza sifa za kufanya hivyo.

"Hakuna kikwazo chochote kwa mtu ambaye atakuwa amekatwa katika michakato ya urais, ubunge na udiwani kutoka katika chama kingine kuja kugombea katika ACT-Wazalendo, taratibu zetu zinasema mtu atatangaza nia, atachukua fomu na atashindana.

"Ukishakuwa mwanachama wa ACT-Wazalendo, unapimwa katika usawa na wanachama wengine, hakuna mwanachama wa miaka sita na mwanachama wa wiki mbili, wote wanapimwa kuwa ni wanachama sawa isipokuwa tutajitahidi kuwa makini kwa uzoefu tulioupata kutoka nyuma kwa maana ya kuangalia rekodi za wahusika.

"(Tunaangalia) nini kimewatoa katika chama husika na chama chetu kinaweza kuathirika vipi iwapo kikimpa nafasi mtu huyo kwenye nafasi fulani. Tutakuwa na uchunguzi wa kina zaidi kuliko ilivyokuwa 2015 kwa sababu katika miaka hii mitano, kumekuwa na matukio ambayo yamebomoa sana imani ya watu katika siasa za vyama vingi," alifafanua.

Membe (66), aliingia katika mgogoro na chama chake baada ya sauti inayodaiwa ya Waziri huyo wa zamani wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kuvuja katika mitandao ya kijamii akiikosoa serikali.

Aliitwa na kuhojiwa na kamati ya maadili ya chama hicho pamoja na makada wengine na waliowahi kuwa viongozi wa juu wa chama hicho; Kanali mstaafu Abdulrahaman Kinana na Yusuph Makamba, waliowahi kuwa makatibu wakuu wa chama hicho.

Februari 28 mwaka huu, Kamati Kuu ya CCM iliazimia Membe kufutwa uanachama wa chama hicho kwa kile kilichoelezwa na Katibu Mwenezi, Humphrey Polepole, kuwa amekuwa na mwenendo usiofaa tangu 2014 na amewahi kupewa adhabu mbalimbali ambazo hazijasaidia kumbadilisha.



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika wilaya ya Ngara, mkoani Kagera, Denice Minja akiwa amebeba mtoto baada ya kumwokoa kutoka katika shimo la choo cha Shule ya Msingi Murgwanza, wilayani humo juzi. **PICHA: LILIAN LUGAKINGIRA**

# Akutwa amekufa kwenye gari

**Na Julieth Mkireri, CHALINZE**

JOHNSON Mtui, amekutwa akiwa amekufa kwenye gari lililokuwa limeegeshwa pembeni mwa barabara katika eneo la Kibiki, Wilaya ya Kipolisi Chalinze.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema tukio hilo lilitokea Mei 21 mwaka huu majira ya saa 1.30.

Alisema gari hilo lenye namba za usajili 515 DSM/ T996 DSE aina ya Scania lililokuwa linatokea Dar es Salaam kwenda Kahama, lilikuwa na mzigo.

Kamanda Wankyo alisema polisi waligundua mwili huo baada ya kuona mwanaume akiruka kutoka katika gari hilo na kukimbilia porini na kuliacha likiwa linanguruma pembezoni mwa Barabara ya Morogoro.

"Kitendo hicho ndicho kilichofanya polisi kusogelea gari hilo na kulifanyia upekuzi ambapo mwili wa marehemu ulikutwa katika kiti cha nyuma ya gari hilo ukiwa na majeraha katika maeneo mbalimbali ya mwili wake kwa kitu chenye ncha kali," alisema.

Kamanda Wankyo aliongeza kuwa mwili ulipofanyiwa upekuzi, ulikutwa na leseni ya udereva ambayo ilikuwa inaonyesha jina la Johnson Mtui.

Alisema kwa sasa wanaendelea na upelelezi kuhusiana na tukio hilo huku akitoa wito kwa mwananchi atakayepata taarifa kuhusiana na tukio hilo, kutoa taarifa katika kituo chochote cha polisi.

# Mitihani kidato cha sita kuanza Juni 29

**Na Waandishi Wetu, DODOMA**

SERIKALI imesema mitihani ya kidato cha sita nchini itaanza Juni 29 na kukamilika Julai 16, mwaka huu na itaenda sambamba na mitihani ya ualimu huku wanafunzi wakitakiwa kufika shuleni kwa wakati.

Pia, imewaagiza viongozi wa mikoa, wilaya na shule za kidato cha sita kuchukua tahadhari zote za afya ikiwamo kuhakikisha wanafunzi wote wanavaa barakoa na wa bweni kulala kwa umbali ili kujiepusha na maambukizo ya ugonjwa wa corona.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alizitaka shule kufanya maandalizi ya kupokea wanafunzi hao Juni mosi, mwaka huu, huku akiwataka wa shule za bweni kuripoti Mei 30, mwaka huu.

Kuhusu tahadhari zitakazochukuliwa kwa wanafunzi wa bweni, kwa vitanda vya dabo deka, atatakiwa kulala mwanafunzi mmoja, bweni linalochukua wanafunzi 80, litatakiwa kuweka wanafunzi 40 na bweni lenye vitanda vilivyobanana, vitatakiwa kutenganishwa.

Kadhalika, aliagiza Baraza la Mitihani la Taifa (Necta) kusambaza ratiba ya mitihani hiyo mara moja, na kuhakikikisha matokeo yanatoka kabla ya Agosti 30, mwaka huu, ili wanafunzi watakaofanya vizuri wapate muda wa kutuma maombi vyuo vikuu bila kuathiriwa na muda.

Alisisitiza kuwa shule ambazo zinafunguliwa hivi sasa ni zenye wanafunzi wa kidato cha sita pekee.

"Kuhusu madarasa mengine utaratibu wao utaelekezwa baadaye, hivyo asije akatokeza mwanafunzi mwingine wa kidato cha kwanza au cha pili na vingine ambavyo havijaelekezwa kurejea shuleni," alisema.

Kuhusu mikopo, Prof. Ndalichako alisema Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Vyuo Vikuu tayari ina fedha kiasi cha Sh. bilioni 122.8 kwa ajili ya wanafunzi wenye sifa ya kupata mikopo hiyo.

"Kinachotakiwa ni vyuo kuwasilisha nyaraka muhimu na hadi Mei 28, mwaka huu, nyaraka hizo ziwe zimewasilishwa Bodi ya Mikopo ili itoe fedha hizo mara tu wanafunzi wanapofika vyuoni," alisema.

Aliviagiza vyuo kupitia mabaraza na Seneti kufanya maandalizi muhimu ili kufungulia kama alivyoagiza Rais John Magufuli.

Alivitaka vyuo kuhakikisha masomo yanaendeshwa katika mfumo ambao unafidia muda ambao wanafunzi wameupoteza kutokana na corona.

"Lazima ratiba zibadilike ili kuwa na muda zaidi wa kusoma kwa lengo la kufidia muda ambao umepotea na kwa vyuo vikuu na vya kati ziwasilishe utaratibu huo kwa mamlaka husika ambayo ni Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (Nacte), ifikapo Mei 27, ili serikali ione kilichopangwa na kufahamu ratiba ya kila chuo na kujipanga kikamilifu kupitia bodi ya mikopo," alisema.

Prof. Ndalichako alivitaka vyuo na shule kuchukua tahadhari ili wanafunzi wanaporudi wasije wakawa sababu ya kurudisha mlipuko wa ugonjwa huo.

"Vyuo na shule lazima viwe na sehemu za kunawia mikono hasa katika maeneo yanayoingiza wanafunzi wengi, madarasani, mabwalo na kumbi za mikutano na kuhakikisha utaratibu huo unatumika kikamilifu," alisema.

Waziri huyo alisema serikali inaandaa mwongozo mahsusi kwa ajili ya vyuo na shule na amefanya mazungumzo na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, na kumwagiza Mganga Mkuu wa Serikali, kuandaa mwongozo huo.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) anayeshughulikia Elimu, Mwita Waitara, alisisitiza shule kuhakikisha wanafunzi na walimu wanavaa barakoa na kunawa mikono kwa maji tiririka kwenye maeneo yote ya kuingilia shuleni na madarasani.

Aliagiza viongozi hao wa mikoa na wilaya kabla ya shule hizo kufunguliwa Juni mosi wakague na kuhakikisha mazingira rafiki yanakuwapo.

"Kuna uwezekano wazazi wakaingia gharama kidogo maana wanapaswa kuwanunulia barakoa lakini na watakaoweza kuwanunua vitakasa mikono ili kujikinga na ugonjwa wa Corona,"alisema.

Alisema walimu waandae wanafunzi kisaikolojia ili wafanye vizuri kwenye mitihani yao.

"Wanafunzi wanaweza kwenda na tangawizi na hata kujifukiza pia ruksa na wanafunzi wote lazima wapimwe joto, na wale wenye mahitaji maalum watakuwa na usimamizi mahususi na ikitokea dalili zozote tutachukua hatua,"alisema.

Alisisitiza kuwa wanafunzi wanapaswa kuripoti shule kwa muda uliopangwa na kutakuwa na adhabu za utoro kwa ambao hawataripoti kwa wakati.

"Kila siku tutakuwa tunapata taarifa na viongozi wa mikoa na wilaya wanawajibu wa kuzunguka kila siku,"alisema.

• ***Imeandikwa na Augusta Njoji na Renatha Msungu***

HABARI KITAIFA

# Ripoti ya CAG moto bungeni

Na Gwamaka Alipipi, DODOMA

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), imezua balaa baada ya Bunge kuitaka serikali kuchukua hatua za kisheria, kinidhamu na kiuwajibikaji dhidi ya wahusika wa ubadhirifu wa fedha za umma.

Akiwasilisha bungeni jana taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), kuhusu taarifa za ukaguzi za CAG, Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Aeshi Hilary, alisema hatua stahiki zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya watuhumiwa waliotajwa kufanya ubadhirifu katika ripoti hiyo.

Alisema Bunge linapendekeza serikali ichukue hatua za kisheria, kinidhamu na kiuwajibikaji kwa wahusika watakaothibitika kufanya ubadhirifu wa fedha za umma ambao walitajwa na CAG.

Aeishi alisema tathimini ya ufanisi wa Mamlaka ya Mapato (TRA), inaonyesha serikali inapaswa kuboresha hali ya utendaji wa vyombo vinavyotoa uamuzi kuhusu mashauri ya kodi kwa kutenga na kutoa fedha na rasilimali nyinginezo kwa wakati, ili kuwezesha uhitimishaji wa mashauri ya kikodi kwa wakati.

Alisema serikali pia inatakiwa iiwezeshe TRA kuwa na uwezo wa kushughulikia mashauri ya kikodi na ukusanyaji wa madeni ya kodi na kodi zilizokadiriwa.

Kiongozi huyo wa PAC pia aligusia malipo yasiyo na manufaa ya Sh. bilioni 1.082 yaliyofanywa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA) kwenda kwa Kampuni ya SMEC INTERNATIONAL PTY Ltd, akisema Bunge linaitaka serikali ifanye uchunguzi wa kina kuhusu malipo hayo ambayo yana viashiria vya ubadhirifu na matumizi mabaya ya madaraka na kuchukua hatua stahiki.

Kuhusu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Aeishi alisema: "Bunge linaazimia kwamba, NIDA iimarishe udhibiti wa ndani kwa kuwa na kumbukumbu sahihi za mahitaji halisi ya malighafi, ili kufanya ununuzi kwa kuzingatia mahitaji halisi kwa kipindi kifupi, kuingia mikataba na taasisi zote zinazotumia taarifa zake ili kuongeza mapato ya serikali na udhibiti wa taarifa za serikali."

PAC pia ilizungumzia deni la Sh. bilioni 454.4 ambalo Shirika la Umeme (Tanesco) linadai taasisi za umma na serikali, akishauri menejimenti ya shirika kuimarisha mikakati ya ukusanyaji wa madeni ili kuhakikisha madeni husika yanakusanywa kwa wakati.

Alisema serikali pia ichukue jitihada mahsusi za kibajeti kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha taasisi zote za serikali zinazodaiwa, zinalipa madeni yao.

Kuhusu Kampuni ya Pride Tanzania kuwa na matumizi mabaya, Aeshi alisema: "Bunge linaazimia kwamba, serikali itekeleze kikamilifu mapendekezo yote yaliyotolewa na CAG katika ukaguzi maalum wa kampuni ya Pride, ili kuendelea kuimarisha udhibiti na uwajibikaji katika fedha za umma."

PAC pia iligusia upungufu uliobainika katika hesabu za Wizara ya Maliasili na Utalii, ikiitaka izingatie kwa ukamilifu matakwa ya sheria na kanuni za fedha za umma na ihakikishe shughuli zinazotekelezwa, ziwe zimekasimiwa kwenye bajeti ya mwaka husika.

Alisema Bunge linamtaka CAG kwa mamlaka yake ya kikatiba na kisheria, aendelee na ukaguzi maalum anaofanya kuhusu utaratibu uliotumika kukusanya fedha, matumizi yake na tathmini ya faida iliyopatikana kwa matumizi husika.

**WABUNGE WACHARUKA**

Akichangia hoja hiyo, Mbunge wa Tanga Mjini (CUF), Musa Mbarouk, alihoji matumizi mabaya ya fedha za Wakala wa Umeme Vijijini (REA) Sh. bilioni 1.082 kwa Kampuni ya SMEC INTERNATIONAL PTY, licha ya kutokufanya kazi huku serikali ikiajiri kampuni 27 kwa ajili ya kusimamia miradi hiyo.

"Rea walikuwa na miradi katika vijiji 1,798, lakini wakamwajiri Mhandisi Mshauri, kwa bahati mbaya kabla hajatoa taarifa, wenzetu wakaajiri kampuni 27, huu ni ubadhirifu mkubwa sana kwa fedha za serikali na kuna viashria vya rushwa, serikali iliangalie jambo hili,"alisema.

Mbunge wa Kilindi (CCM), Omari Kigua, alisema serikali imekuwa ikikosa mabilioni ya shilingi kutokana na TRA kushindwa kukusanya mapato.

"Niiombe serikali ihakikishe bodi zinakutana ili ziweze kukusanya mapato, TRA wakisimama vizuri, serikali itaweza kusimamia miradi ya kimkakati," alisema.

Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashid Shangazi, alisema TRA inahitaji maboresho husussani katika mashauri ya ukusanyaji kodi kwa kuwa mifumo imekuwa haifanyi kazi kwa wakati, hivyo kuikosesha serikali mapato.

"TRA inahitaji maboresho hasa mashauri mengi ya kikodi kutoamuliwa kwa wakati, ukichunguza mifumo haifanyi kazi kwa haraka, tunaomba Wizara ya Fedha na Mipango kuweka msukumo katika jambo hili," alisema.

Mbunge wa Mwanakwerekwe (CCM), Ali Salim Khamis, alihoji sababu za Benki Kuu (BoT) hatokagua noti chakavu za Sh. bilioni 300 ambazo walipewa na benki za kibiashara.

"Fedha chakavu zaidi ya Sh. bilioni 300 hawakuzikagua wala kuziangalia ambazo ni noti wamepewa na benki za biashara na inawezekanaje bilioni 300 ziwe feki, inawezekanaje?

"Leo BoT inakaa na Sh. bilioni 300 halafu kibaya wanatoa na penati wakati fedha hawajazikagua, jambo hili liangaliwe," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Felister Bura, alihoji matumizi ya Sh. bilioni 1.5 zilizotumika katika Wizara ya Maliasili na Utalii bila ya utaratibu maalum.

"Bilioni 1.5 zilizotumika kwa ajili ya sekta ya utalii, fedha hizo hazikuidhinishwa na Bunge na kibali walichopata, walipata baada ya matumizi.

"Wangeomba kibali cha matumizi wapate kabla ya matumizi. Inaelekea hizi fedha zilitumika kabla ya kibali, ninaiomba serikali wafuate matumizi ya hizi fedha, ili malalamiko haya yasiwapo,"alisema.

# Polepole: CCM ina ushahidi makada walioanza kampeni

Na Elizabeth Zaya

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimetangaza kiama kwa wanachama wake walioanza kufanya vurugu za kampeni za chinichini kutafuta uongozi kwenye majimbo na kata kabla ya chama hicho kutoa tangazo rasmi la kuanza kampeni.



Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Taifa, Huphrey Polepole, alisema kiama hicho hakitawahusu tu wanachama, bali pia viongozi wa serikali ambao pamoja na kwamba wako kwenye nafasi za kutumika, wamekuwa wakijipenyeza kufanya vurugu hizo za kutaka majimbo.

Polepole alisema tayari wana ushahidi wa sauti, video, picha na barua za malalamiko za baadhi ya wanachama na viongozi ambao wamekuwa wakifanya harakati hizo.

"Chama kinaendelea kuwakumbusha wanachama kuwa tutumie muda huu kufuata Katiba ya CCM na kanuni, tunapenda wanachama watakaopenda kuomba dhamana ya uongozi, wafahamu kwamba uongozi hautafutwi, uongozi mtu hupewa, yule anayestahili.

"Hivyo, chama kinatambua na kinawafahamu wote wanaofanya vurugu kwenye majimbo ya uchaguzi na kata, tuna ushahidi wenu wa sauti, video, picha, barua za malalamiko na ninataka kuwatangazia kwa niaba ya CCM kwamba, wavurugaji wote na walioanza kampeni kabla ya wakati, hawatapewa dhamana ya uongozi kwenye chama.

"Hii inakwenda sambamba na baadhi ya watumishi wetu kwenye serikali ambao pia wamekuwa wakifanya hivyo kwenye majimbo. Ukipewa kazi kwenye serikali na Rais, hebu tenda hiyo kazi mpaka ikamilike ili na vitu vizuri vionekane, ili kumshawishi aliyekupa kama anayo nyingine akupe tena," alionya.

Polepole alisema chama hicho kinaamini kwamba binadamu wote ni sawa, hivyo kitatoa ruhusa ya kila mwanachama kuomba ridhaa hiyo mpaka pale kitakapotangaza rasmi na kwamba hakitamtambua mwanachama au kiongozi yeyote atakayethibitisha kuanza kampeni hizo kabla ya muda.

Polepole alisema tayari chama hicho kimeandaa kituo cha taarifa za uchaguzi ambacho pia kitatumika kupokea taarifa zile zitakazohusu wanaofanya vurugu kabla ya muda.

Polepole pia alisema mchakato wa kuandika ilani ndani ya chama hicho umekamilika na hivi karibuni baada ya vikao vya chama watatangaza.




**Bonite Bottlers Ltd** inayo furaha kuwaletea **Maji ya Kilimanjaro katika ujazo mkubwa wa LITA 6, LITA 12 na LITA 18.9.** Tumewekeza katika mitambo ya kisasa ya kuzalisha maji katika ujazo mkubwa ili kuwawezesha wateja, wanywaji na wadau wetu kupata maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, maofisini na kwenye taasisi mbalimbali.

**UPATIKANAJI:-**

- Maji ya Kilimanjaro katika ujazo mkubwa yanapatikana kwenye depoti zetu zote zilizoko mikoani, maduka na wauzaji wa jumla nchi nzima.
- Kwa Wateja wetu wa Mkoa wa Dar es Salaam, unaweza kununua maji ya kunywa ya Kilimanjaro ukiwa nyumbani kwa njia ya mtandao kupitia makampuni ya usambazaji bidhaa tunayoshirikiana nayo ambayo ni Shoponline Tanzania **www.shoponline.co.tz** na Piki Deliveries **www.piki.co.tz** .

Ni matumaini yetu mtaendelea kutuunga mkono kwa kuburudika na maji kutoka kilele cha Afrika.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI:**

**Moshi:** +255 755851170 au +255 27 2754422/7, **Arusha:** +255 756339532 au +255 27 2544876, **Dar:** +255 754635988 au +255 22 700450/655, **Morogoro:** +255 782546090, **Dodoma:** +255 787495439, **Karatu:** +255 757673123, **Babati:** +255 765459199, **Singida:** +255 755271963, **Tanga:** +255 763407979, **Mbeya:** +255 757266235, **Mwanza:** +255 742099191, **Nzega:** +255 746031412

**MAJI YA KUNYWA YA KILIMANJARO NI MAJI YA KUAMINIKA KILA SIKU!**

# Wabunge Chadema watangaza kuhamia NCCR-Mageuzi

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

WABUNGE wawili wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), wametangaza kujiunga na Chama cha NCCR-Mageuzi baada ya Bunge la 11 kuvunjwa huku wakikituhumu chama hicho kwa kuvunja misingi ya Katiba.

Wabunge hao waliotangaza kukihama chama hicho ni Joyce Solkombi na Susanne Maselle wa Viti Maalum.

Wakizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, walisema wamehama Chadema kutokana na kutoheshimika kwa Katiba ilhali ndio msingi mkuu wa kuanzishwa kwa mageuzi nchini.

Madai mengine ni kukiukwa kwa haki ya kusikilizwa kabla ya kuhukumiwa na kutoa mfano kwa wabunge wanne walioondolewa wakiwamo Wilfred Lwakatare, Joseph Selasini, Anthony Komu na David Silinde, ambao wote walifukuzwa uanachama bila kusikilizwa.

"Natural Justice (usawa wa haki) iko wapi hapo wakati haki hiyo ipo ndani ya katiba ya chama hiki ambacho leo hii wabunge wake wanafukuzwa bila kupewa nafasi ya kusikilizwa," walihoji.

Kadhalika, walisema sababu nyingine ni kukiukwa haki ya kuhoji matumizi ya michango na fedha za ruzuku na kutoa mfano kwa wabunge wa viti maalumu kila mmoja kwa mwezi walikuwa wanachangia chama Sh. 1,550,000 tangu Januari 2016 mpaka Aprili 2019, ambazo matumizi yake hayafahamiki.

"Ndani ya miezi 40 kila mmoja wetu amechangia chama takriban Sh. milioni 62, wabunge wa viti maalum tupo 37, hivyo tumechangia zaidi ya Sh. bilioni 2.2, hoja yetu hatulalamiki kuchangia hapa chama bali ni wajibu wetu kuhoji fedha hizi matumizi yake hayajawahi kuwekwa wazi na haturuhusiwi kuhoji popote."

Walidai kuwa chama kimekuwa kikihodhiwa madaraka yake kwa wabunge wachache na wengi wao ni wanaume na hivyo kuwapo kwa mwanya wa unyanyasaji wa kijinsia na kingono.

Wabunge hao walidai hoja zingine ni kuwapo ndani ya chama hicho mgawanyiko mkubwa unaotokana na baadhi ya watu kujiona wao ni bora kuliko wengine na jitihada za kutaka kuondokana na hali hiyo kipindi cha kuelekea kwenye uchaguzi mkuu zimeshindikana.

Vile vile, walidai kuwa ndani ya chama hicho kuna makundi ya kibaguzi hadi bungeni na kutaja upande wabunge wa viti maalum uchangiaji katika vikao vya bunge unaenda kwa kufahamiana na wengine kufanywa wapiga makofi na kuitwa wabunge maarufu (Super Star).

Walidai sababu zingine zilizowavutia kuhamia NCCR- Mageuzi ni mfumo wa kuendesha chama kitaasisi, na itikadi yake ya utu ambao msingi wake mkuu ni haki za binadamu.

Pia, walisema katiba yake imewekwa wazi usawa wa jinsia kwa viongozi wakuu wa juu kama Makamu Mwenyekiti wa Taifa na Katibu Mkuu ni wanawake huku katiba na kanuni za uendeshaji wa chama zimeziba mianya ya uvunjifu wa amani ndani ya chama na nje kwa maslahi ya kulinda amani ya nchi.

Walisema chama kimekuwa na utulivu wa kisiasa kwa kuweka maslahi ya taifa mbele kabla ya mengine, ikiwa ni kujikita kwenye kuboresha elimu kwa Watanzania kwa hoja na vitendo.




Meneja miradi wa jumuiya vijana ya Nyota Njema, Ismail Hassan (kushoto), akikabidhi msaada wa vyakula mbalimbali kwa Mwakilishi wa kituo cha watoto yatima cha Ally Bin Abumutwalib, kilichopo Chanika, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MOSHI LUSONZO**

# Manyanya atangaza fursa soko la samaki

**Na Eliud Rwechungura**

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya, ametangaza fursa za soko la samaki Kanda ya Ziwa wakati wa mapokezi ya ndege ya Ethiopia Airlines iliyoanza safari zake kuja Tanzania katika mkoa wa Mwanza kuchukua minofu ya samaki ambayo inauzwa katika nchi mbalimbali duniani.

Manyanya amesema: "Mpaka kufikia Machi, 2020 samaki tani 392,933 wamevunwa nchini na mauzo yameongezeka kulinganisha na miaka miwili iliyopita na mauzo yalikuwa Sh. bilioni 379 na kufikia bilioni 691.88 kwa mwaka 2018/2019. Tani 32,388.88 zenye thamani ya Sh. bilioni 436.97 ziliuzwa nje ya nchi na mapato kwa serikali yalikuwa bilioni 19.1"

Baada ya kushuhudia ndege hiyo ikipakia samaki amewatangazia na kuwadhihirishia wawekezaji wote nchini kuwa kuna soko la samaki la uhakika kwasababu kwa sasa samaki wanafuatwa moja kwa moja mkoani Mwanza na kupelekwa katika maeneo mbalimbali duniani.

"Tanzania tumejaliwa, tunao samaki wazuri na wakutosha na sio Ziwa Victoria pekee tuna maziwa mengine makubwa na Bahari ya Hindi, kwa hiyo naomba niwadhihirishie wawekezaji wote kuwa sasa tuna soko la uhakika la samaki, jitokezeni kuwekeza kwasababu minofu yetu ya samaki inafuatwa moja kwa moja na ndege hadi Mkoa wa Mwanza."

Vile vile, alisisitiza ndege ya Ethiopia iliyoanza kuingia nchini juzi imepakia kilogramu 17,262 zenye thamani ya Sh. 191,874,837.78 na mrabaha uliolipwa ni Sh. 9,541,301.21 na samaki watauzwa katika nchi za Belgium, Uholanzi, Ujerumani, Ufaransa, Ureno na Australia na kwa upande wa mabondo (fish maws) soko kubwa ni China.

Naye Naibu wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi, Atashasta Nditiye, alisema kuwa safari za ndege ya Ethiopia kuja kuchukua samaki Mwanza ni fursa kubwa kwa wana Mwanza na Kanda ya Ziwa kwa ujumla kwa kuwa kabla ya hapo ilikuwa inakuja ndege ya Rwanda Air mara moja kwa wiki kila Jumanne.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, amesema viwanda vitatu vimesafirisha samaki juzi na kuvitaja kuwa Kiwanda cha Victoria Perch limited ambao wamesafirisha tani 5.4 (5,400kg) zenye thamani ya Dola za Marekani 21,600) Kiwanda cha Nile Perch Limited ambacho wamesafirisha tani 8.9 (8990kg), zenye thamani ya Dola za Marekani 35,900 na Kiwanda cha Omega Fish limited kinachosafirisha tani tano (5,000kg) zenye thamani ya Dola 22,320.

Mongella alisisitiza kuwa uzalishaji wa Kanda ya Ziwa kwa wastani kila wiki katika kipindi cha mavuno ni tani 1,100 na kipindi mavuno haba ni tani 220.

# Kaya 5,000 kunufaika msaada wa chakula

**Na Mary Geofrey**

KAYA 5,000 za watu wasiyojiweza, walemavu, yatima na wajane, zinatarajia kunufaika na misaada ya chakula kutoka taasisi ya Nama kupitia washirika wake, Annahl Trust na Nice Tanzania.

Imeelezwa kuwa, misaada hiyo yenye thamani ya Sh. milioni 800, itatolewa kwa wakazi wa Dar es Salaam, Pwani na Visiwani Zanzibar kwa lengo la kuunga juhudi za serikali katika kukabiliana na janga la corona.

Mratibu wa misaada hiyo wa Taasisi ya Nama, Hamza Jabir, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuwa misaada hiyo itajumuisha pia msaada wa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 500.

"Taasisi hizi zimeamua kushirikiana kuunga mkono juhudi za serikali katika kupambana na maambukizo ya Corona kwa Watanzania, hivyo tutatoa msaada wa Sh. bilioni 1.3 unaojumuisha vifaa tiba na chakula kwa familia zisizojiweza," aliahidi.

Jabir alibainisha kuwa, misaada ya chakula watakayotoa ni mchele kilo 10, unga kilo 10, sukari, mafuta, vitakasa mikono na barakoa kwa kila familia yenye uhitaji.

Kuhusu vifaa tiba, alisema watatoa mavazi ya kujikinga kwa watoa huduma (PPEO, Oxymeter, oxygen concentrator, Thermoscanner, vitanda vya chumba cha uangalizi maalum (ICU) na vingine vinavyohitajika kwa kuzingatia miongozo wa serikali na Wizara ya Afya.

"Utekelezaji wa utoaji misaada hii utaanza Mei 27 na kuendelea na kwa mtaa wa Mwananyamala pekee, tutazifikia kaya 200 na tutashirikiana na viongozi wa jamii na serikali hasa katika kuzitambua kaya zinazolengwa katika maeneo yote," alisema.

Mratibu mwenza wa shughuli hiyo, Seleman Abdallah, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwapa ushirikiano.

"Tunaishukuru Taasisi ya Nama Foundation kwa kutambua juhudi za serikali na washirika wake An-Nahl na Nice Tanzania ambao ni wadau wakubwa katika kusaidia jamii.

"Tuendelee kuunga mkono serikali na kupongeza kwa juhudi zake kuisadia jamii na kufikia jamii kubwa ya Watanzania itakapopata uwezo zaidi," Abdallah alisema.

# Marekani yatoa bil. 5.6/- kusaidia afya TZ

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Marekani imetangaza kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa (Usaid), kuongeza Dola za Kimarekani milioni 2.4 (Sh. bilioni 5.6), ikiwa ni msaada kwa sekta ya afya Tanzania.

Msaada huo unalenga kuimarisha uwezo wa maabara na upimaji wa kimaabara, kusaidia jitihada za utoaji taarifa, miradi ya maji na usafi wa mazingira, kuzuia na kudhibiti maambukizo, kutoa elimu ya afya kwa umma na miradi mingine.

Taarifa iliyotolewa na Ubalozi wa Marekani jana, ilisema fedha hizo ni nyongeza ya msaada wa Dola za Kimarekani milioni moja, unaolenga kusaidia mapambano dhidi ya janga la Covid-19, uliotolewa hivi karibuni na kufanya kiasi kipya cha fedha zilizotolewa kwa Tanzania ili kukabiliana na janga hilo kufikia Dola milioni 3.4.

Kiasi kingine cha Dola milioni 1.9 zimebadilishwa matumizi na kuelekezwa kwenye mapambano dhidi ya janga hilo.

"Hii inafanya jumla ya fedha zote zilizotolewa na Marekani katika kukabiliana na Covid-19 nchini Tanzania hadi hivi sasa kufikia Dola za Kimarekani milioni 5.3 (Sh. bilioni 12.2)," ilisema taarifa hiyo.

"Katika kipindi cha miaka 20 iliyopita, Marekani imewekeza zaidi ya Dola za Kimarekani bilioni 7.5 kwa maendeleo ya Tanzania huku karibu Dola bilioni 4.9 zikielekezwa kwenye sekta ya afya pekee. Toka mwaka 2009, Serikali ya Marekani imetoa zaidi ya Dola bilioni 100 kusaidia miradi ya afya na takriban Dola bilioni 70 kama msaada wa kibinadamu duniani kote," iliongeza taarifa hiyo.

Serikali ya Marekani inaendelea kuwa mfadhili mkubwa zaidi duniani wa miradi ya afya na shughuli za kibinadamu zinazolenga maendeleo ya muda mrefu na jitihada za washirika wake kujijengea uwezo na kuchukua hatua za dharura wakati wa majanga.

"Tunaongoza duniani katika utoaji wa misaada ya kibinadamu na kiafya katika kukabiliana na janga la Covid-19," iliongeza taarifa hiyo.

Watu wa Marekani wametoa zaidi ya Dola bilioni 10 zitakazosaidia jitihada za kimataifa zakukabiliana na Covid-19. "Tutaendelea kuhakikisha kuwa mchango mkubwa wa kifedha na wa kisayansi wa Marekani katika mapambano haya unabaki kuwa kitovu na sehemu ya jitihada za pamoja na zilizoratibiwa vyema za jumuiya ya kimataifa dhidi ya Covid-19. Ikiwa ni miezi kadhaa sasa tukipambana na janga hili nchini kwetu na nje ya nchi yetu, Marekani inaendelea kuongoza jitihada za kimataifa dhidi ya mlipuko huu, ikijenga katika uzoefu wa miongo kadhaa ya uongozi katika utoaji misaada ya kiafya inayookoa maisha na misaada ya kibinadamu."



Baadhi ya wanafunzi shule za mkoa wa Dodoma, wakifurahia wakati wa Jukwaa la Kipepeo, lililofanyika jijini huo, mapema wiki hii, lenye dhumuni ya kutoa elimu ya mimba za utotoni na maambukizo ya Ukimwi. Kampeni hiyo, ipo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na kudhaminiwa na Global Fund, NACP, Taasisi ya Benjamin William Mkapa na kuratibiwa na Clouds Media Group. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ummy amuahidi makubwa JPM

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amemuahidi, Rais John Magufuli kuwa ataendelea kuitumikia nchi kwa bidii, uaminifu na maarifa zaidi.

Hatua hiyo inakuja ikiwa ni siku moja tangu Rais Magufuli kumwagia sifa waziri huyo kuwa katika janga la virusi vya corona, amejituma na kuchapa kazi licha ya kwamba hana taaluma ya udaktari.

Juzi, wakati Rais Magufuli akiapisha viongozi mbalimbali aliowateua, alisema Waziri Ummy alisimamia wizara hiyo kwa ujasiri mkubwa.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Waziri Ummy aliandika: 'Asante Rais Magufuli kwa kuendelea kuniamini na kunitia moyo katika kusimamia sekta ya afya nchini hasa katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya corona'.

"Naahidi kuendelea kuitumikia nchi yangu kwa bidii, uaminifu na maarifa zaidi."

Rais Magufuli alisema Waziri Ummy anajituma katika suala hilo la corona na amesimama licha ya kwamba hana taaluma ya udaktari.

"Kuna wakati fulani niliona anasimama peke yake kwenye wizara, yeye siyo daktari wa kusomea, unajiuliza mwanasiasa anasimama peke yake kuzungumzia taaluma ya udaktari, wasaidizi wake wote ni madaktari huoni matokeo, nakupongeza sana Ummy najua nilikutesa.

"Sitaki kueleza mengi, lakini ni kweli aliteseka kwa sababu kwa siku mara nyingine alikuwa anapigiwa simu zaidi ya mara nane iwe saa nane iwe saa ngapi, unapokuwa kwenye vita saa nyingine kubembelezana hapana."

## Mashahidi 19 kuitwa kesi ya bangi

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri umepanga kuita mashahidi 19 katika kesi ya kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya aina ya bangi kilo 128.54 inayomkabili Gudluck Mbowe na Ally Mtema.

Madai hayo yalitolewa jana na Jamhuri katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Uhujumu Uchumi na Rushwa maarufu kama ya Mafisadi, iliyoketi chini ya Jaji Immacula Banzi.

Wakili wa Serikali Costantine Kakula, alidai kuwa mbali na mashahidi 19, pia watawasilisha na vielelezo mbalimbali ikiwamo mabegi saba ya bangi na gari moja aina ya Toyota IST.

Akiwasomea maelezo ya awali, Kakula alidai kuwa washitakiwa hao walikamatwa Oktoba 15, mwaka 2017 eneo la Kibaha kwa Matiasi baada ya polisi kupewa taarifa kwamba watu hao wamebeba dawa hizo za kulevya.

Ilidaiwa kwamba, washitakiwa walibeba mabegi saba ya bangi katika gari lao aina ya Toyota IST.

Pia, ilidaiwa kuwa siku ya tukio, polisi eneo la Kibamba walijaribu kusimamisha gari hilo, lakini hawakusimama na dereva aliendelea kuendesha kwa mwendo kasi.

Polisi walikimbiza gari hilo hadi lilipoingia mtaroni na kupata ajali na washitakiwa walikamatwa na upekuzi ulipofanyika.

Upekuzi huo ulihusisha washitakiwa pamoja na shahidi wa kujitegemea na kufanikiwa kukamatwa kwa mabegi saba ya bangi.

Hati ya upekuzi ilijazwa na kusainiwa na washitakiwa pamoja na shahidi huyo. Katika mahojiano washitakiwa hao walikiri kubeba dawa hizo za kuevya.

Ripoti ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilithibitisha kwamba mzigo huo ni dawa za kulevya aina ya bangi kilo 128.54.

**Pia, ilidaiwa kuwa siku ya tukio, polisi eneo la Kibamba walijaribu kusimamisha gari hilo, lakini hawakusimama na dereva aliendelea kuendesha kwa mwendo kasi.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu zakumbushwa Fair Play lala salama Ligi Kuu

**RAIS** John Pombe Magufuli juzi alitangaza rasmi kufungua michezo yote hapa nchini kuanzia Juni Mosi, mwaka huu.

Kauli hiyo inaashiria kurejea kwa michezo yote iliyokuwa imesimama tangu Machi 17, mwaka huu ili kupisha maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19).

Hata hivyo, inaonekana kama Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ni maarufu nchini ndio pekee ilisimama, lakini ukweli zilisimama pia ligi nyingine ikiwamo Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili, Ligi ya Wanawake na mashindano ya Kombe la FA.

Ligi Kuu ndiyo inayotoa wawakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wakati Kombe la FA hutoa mwakilishi wa michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Pia Ligi Kuu Zanzibar ambayo hutoa wawakilishi wa mashindano hao ya kimataifa yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) na ligi nyingine ndogo zinazochezwa visiwani humo, pia zilisimamishwa kwa sababu ya kujikinga na ugonjwa huo ambao umeua maelfu ya watu duniani.

Kurejea kwa ligi hizo sasa kunatoa taswira kuwa bingwa atakayepatikana au atakayetangazwa atakuwa ni yule aliyefanya vizuri zaidi uwanjani na si mezani kama baadhi ya mataifa yalivyoamua kumaliza msimu wa 2019/20.

Kauli ya JPM ni dhahiri sasa inategua kitendawili cha timu zipi zinastahili kwenda kupeperusha bendera ya Tanzania katika mashindano ya kimataifa kwa mujibu wa kanuni zilizopitishwa na kukubaliwa na klabu zote.

Lakini mbali na viongozi walivyokuwa wanaumiza kichwa kuhusiana na wawakilishi hao watakavyopatikana endapo ligi hizo hazitarejea na kumalizika kama zilivyotarajiwa, pia kulikuwa na hoja mbalimbali kuhusiana na timu zitakazoshuka daraja.

Wadau wengi walionekana kutoa ushauri katika kuteua wawakilishi wa nchi watakaokwenda kushiriki kwenye mashindano yanayoandaliwa na CAF, lakini wakitaka kuzionea huruma zile zinazotakiwa kushuka daraja kwa kueleza, timu zote ziendelee.

Hata hivyo wadau hao hao wanasahau pia katika ligi za madaraja ya chini, kuna klabu ambazo zinatakiwa kupanda daraja ikiwamo Gwambina FC ya jijini Mwanza, hata ikifungwa kwenye mchezo wake wa mwisho, haitaathiri nafasi yake ya kuwania kupanda daraja, kwa sababu tayari ilikuwa imeshamaliza kampeni yake.

Nipashe inapenda kulipongeza Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), na vyama vingine mbalimbali vya michezo kwa kuwa watulivu na kutochukua uamuzi wowote wa haraka katika kumaliza msimu huu na badala yake vilikuwa vikifanya kazi karibu na serikali kufahamu tathmini ya Covid 19 ilivyofikia.

Tunapenda kuwakumbusha mashabiki wote kuendelea kufuata maelekezo yatakayotolewa na wataalamu wa afya wakati ligi na michezo hiyo itakaporejea ili kudhibiti maambukizo ya ugonjwa huo uliotikisa dunia.

Ikumbukwe mbali na michezo kusaidia kuimarisha afya zetu, hutoa ajira kwa mamia ya wachezaji pamoja na wadau wengine ambao shughuli zao hutegemea mechi na mashindano mbalimbali.

Tunawakumbusha ili bingwa apatikane kwa haki pamoja na timu zitakazoshuka daraja, haki inatakiwa kutawala na kuonekana kwa vitendo kwenye mechi zote zilizobakia.

Usimamizi huo ufanyike katika mechi zote na si uangalizi wa kiwango cha juu na usionekana pale vigogo, Simba na Yanga watapokuwa uwanjani. Haki sawa kwa timu zote za Ligi Kuu Bara.

Watanzania tunatakiwa kuendelea kuwa wasikivu kama Rais Magufuli alivyotamka kwa kuhakikisha michezo inarejea na afya za wananchi wote zinaendelea kuimarika wakati wote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba, Yanga zinavyowindana



Na Barnabas Maro

'UTANI' ni desturi za kimila zinazowafanya watu wanaojuana waweze kuambiana au kutengeneza jambo lolote la mzaha bila ya kuleta chuki au kero; maneno ya dhihaka. Tabia ya watu kufanyiana masihara kwa lengo la kuambiana kweli na kuimarisha uhusiano wao.

Kwa Simba na Yanga hakuna mambo kama hayo ila ni chuki, yaani hali ya kutokuwapo upendo; hali ya kuwa na roho mbaya, kuwa na kinyongo na kutotaka maendeleo ya mwingine. Kwa ufupi, kwa sasa, Simba na Yanga si watani wa jadi kama isemwavyo, bali ni maadui. Wanaobisha wabishe tu, lakini huo ndio ukweli wenyewe.

Kwa sababu hiyo, kila moja huiombea nyingine mambo mabaya badala ya mazuri na mema. Kile kisemwacho 'watani wa jadi' si kweli ila ni maneno tu! Watani hawachokozani ili kufanyiana ubaya, kuzomeana na kuchekana bali husaidiana wakati wa shida, tena kwa hali na mali.

Ukitaka kuthibitisha hali hii, subiri wakati wa kipindi cha usajili uone jinsi zinavyochimbana. Kila upande hujitahidi kuwashawishi baadhi ya wachezaji wa upande mwingine ili kuwasajili. Itokeapo upande wa Msimbazi au Jangwani umepata fununu ya mwingine kumsajili mchezaji muhimu, lazima kuwe na tafrani ya aina yake.

Mchezaji huyo huandamwa kwa kila hali, kwa kuahidiwa fedha nyingi na mambo mazuri kuliko aliyoahidiwa na upande mwingine! Hali kama hii yataka mchezaji anayegombewa awe mtulivu na kufanya tafakuri itakayomwezesha kufanya uamuzi sahihi. Aidha anapaswa kuwa makini kwa watu anaowaomba ushauri.

Wanapata nafasi za kucheza au huwekwa kando na kuwa wachezaji wa akiba? Katika hali kama hiyo lazima wapime uwezo wao kama wanawazidi waliopo ama la. Vinginevyo wasikubali kughilibiwa.

Wachezaji waweke wazi kuwa mikataba watakayotia saini zao iwe na kifungu kinachowapa haki na uhuru wa kwenda kufanya majaribio na timu za ughaibuni iwapo watatakiwa. Itazinufaisha vilabu vyetu kwa kuwauza wachezaji wao nnje ya nchi.

Pia wawe waangalifu na mameneja wanaowatafutia timu kwani wanaweza kupewa hela na timu zinazotafuta wachezaji ili kughilibu walipwe hela kiduchu na wakati huo huo kuchukua hela kwa wachezaji wanaotafutiwa timu.

Wahenga walisema "Fedha ilivunja nguu, milima ikalala." Maana yake pesa zina uwezo wa kuvunja milima na vilima. Hii ni methali ya kupigia mfano uwezo wa fedha. Mtu akiwa na pesa anaweza kufanikiwa kufanya mambo ambayo asingeweza kuyafanya wala kudhania kuyafanya.

Kuna chama kilichoundwa na wachezaji wa zamani ili kutetea stahiki (kitendo cha mtu kuwa na haki ya kupata kitu fulani kutokana na ufanisi aliopata) za wachezaji wa sasa. Wachezaji wa zamani ambao sasa waitwa 'zilipendwa' enzi zao walifanya kandanda kama mchezo wa kuwafurahisha watazamaji na wakati huohuo kuimarisha afya zao. Hawakulipwa mishahara kama walivyo wachezaji wa sasa.

Wachezaji hao wanajua matatizo waliyokumbana nao wakati ule. Nadhani ndo sababu ya kuunda chama cha wachezaji ili walipwe mishahara na stahiki nyinginezo, kuwatetea wanapodhulumiwa au kunyimwa haki zao.

Kwa hali yoyote iwayo, chama cha wacheza kandanda hakitakuwa na nguvu bila hela kwani kuna wakati itabidi kuwatumia wanasheria ili kuwatetea wachezaji waliopunjwa/wanaopunjwa stahiki zao na wanaoachwa na vilabu vyao dakika za mwisho na kuwakosesha timu za kuwasajili!

Twaambiwa "Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu." Je, wacheza kandanda wamejiunga na chama chao na kulipa ada za kila mwezi au mpaka wanapopatwa na matatizo ndio wanakumbuka kuwa kuna chama chao cha kuwatetea?

Hata hivyo, ni kama chama cha wacheza kandanda kingali kwenye usingizi mzito kwani hatujaona makucha yake pale wachezaji wanapopunjwa au hata kunyimwa stahiki zao! Hatujasikia kuwaita wanachama (wachezaji) wao kuwaeleza na kuwakumbusha wajibu wao kwa vilabu. Kama chama hicho kipo, mbona hatujasikia hekaheka zake dhidi ya vilabu vinavyowaonea au kuwadhulumu wachezaji wao?

Kwa upande mwingine wachezaji wanapaswa kutambua kuna leo na kesho. Hapana shaka wamesikia au kuona jinsi wachezaji wenzao wanavyohangaika pindi wanapodai fedha za usajili na malimbikizo ya mishahara yao mpaka kupelekana TFF, CAF na FIFA. Kwa hali hiyo wanapaswa kuzinduka na kuona umuhimu wa kujiunga na chama chao.

"Ujinga wa kuuza si ubaradhuli wa kununua." 'Ubaradhuli' ni upumbavu. Ni heri kuwa mjinga wa kuuza kuliko kuwa mjinga wa kununua. Methali hii hutumiwa kuwakumbusha watu umuhimu wa kuwa makini na kutahadhari wakinunuapo au wanapopendezwa na kitu fulani.

*marobarnabas@yahoo.com*
*0784 334 096*

# NFRA wataka ufanisi usimamiaji maslahi wafanyakazi

**Na Mathias Canal, MOROGORO**

BARAZA la Wafanyakazi wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), wametaka ufanisi kazini kusimamia maslahi ya wafanyakazi.

Katika mkutano huo wa siku mbili wafanyakazi wametoa maoni kuhusu umuhimu wa kushirikishwa kwenye shughuli mbalimbali mara kwa mara ili kutambua majukumu yanayofanywa na taasisi hiyo.

Kadhalika, wameomba kuendelea kujengewa misingi ya uwajibikaji hasa katika kutambua wajibu wao kwa umma na kusisitiza kuwa watatekeleza majukumu yao bila uzembe.

Akizindua Baraza hilo juzi, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu wa Wizara ya Kilimo, Hilda Kinanga wakati akimuwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alisema si vema watumishi wakatumia muda mwingi kufanya shughuli ambazo hazina tija zinazoathiri utendaji kazi.

Aliongeza kuwa serikali inayo dhamira ya dhati ya kuondoa uzembe na ubadhirifu miongoni mwa watumishi wa umma na hivyo mtumishi anaruhusiwa kudai haki zile za msingi kwa kuzingatia kanuni, sheria na taratibu za utumishi wa umma wakati wa kutekeleza wajibu wake wa msingi kwa mwajiri na kwa kutumia lugha ya staha.

Wajumbe pia wamejadili masuala mbalimbali yanayohusu wakala na miongoni mwa ajenda hizo ni kupitia Mpango wa Biashara wa mwaka 2020/2021 (Business Plan), taarifa ya utekelezaji ya robo ya tatu ya mwaka 2019/2020 na kupitia Rasimu ya Miundo mipya ya Maendeleo ya Utumishi.

Katika agenda zilizojadiliwa ya kwanza imewapitisha katika malengo/mipango ya wakala, ya pili ni utekelezaji wa majukumu ya wakala uliofanyika kwa mwaka uliopo na tatu ni mpango wa kuboresha maslahi ya wafanyakazi kwa lengo ya kuandaa majukumu mapya yanayoendana na muundo mpya wa taasisi.

Kwa nyakati tofauti katika michango yao wamesisitiza kuwa hakuna haki bila wajibu hivyo wana wajibu muhimu wa kutekeleza majukumu yao na ari kubwa.

"Kwa kutambua uzito na umuhimu wa majukumu hayo, kila mmoja katika sehemu yake ya kazi anatakiwa kuwajibika na kufanya kazi kwa bidii na kwa uadilifu ili kuiwezesha serikali kufikia malengo yake ya kukuza uchumi na kuondoa umaskini kwa wananchi kwa kuwezesha nchi yetu kufikia uchumi wa kati," alikaririwa Meneja NFRA Kanda ya Sumbawanga, Abdillah Nyangasa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), Milton Lupa, alisema kuwa bado Taasisi ina changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu ya kutoa huduma kwa umma ikiwamo ukosefu wa rasilimali fedha na rasilimali watu wa kutosha, hali inayosababisha kutofikiwa kwa malengo.

Aliwahakikishia kuwa serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kutatua changamoto hizo ikiwamo kuiomba iwapatie watumishi ili kukidhi matakwa yao.

Alisisitiza watumishi wote wanapaswa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na maadili katika utumishi wa umma.

Pia, serikali haitasita kuchukua hatua kwa mtumishi yeyote atakayejihusisha na vitendo vya rushwa pamoja na vitendo vinavyokiuka maadili ya utumishi wa umma.



Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri wa Wilaya ya Kondoa, Mustapha Yusuf (kushoto), akizungumza kwenye kikao chake na wadau wa maendeleo ofisini kwake, wilayani humo, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## M/kiti atoa siku 7 kukamilisha nyumba za walimu

**Na Jumbe Ismailly, ITIGI**

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Itigi, wilayani Manyoni, mkoani Singida, ametoa muda wa wiki moja kwa idara ya elimu msingi katika halmashauri hiyo kukamilisha ujenzi wa nyumba mbili za walimu katika shule za msingi Mkajenga na Mahinya.

Ally Minja alitoa agizo hilo wakati wa kufunga mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo.

"Tumesisitiza masuala ya matumizi ya fedha ambazo tumeletewa na serikali kwa ajili ya miradi, kwanza miradi ya ujenzi wa umaliziaji wa nyumba mbili za walimu wa shule za msingi Mkajenga pamoja na shule ya msingi Mahinya,"alifafanua Minja.

Vile vile, aliwaagiza madiwani kwenda kupambana kwenye maeneo yao kwa kipindi cha wiki moja, kuahidi kuwasaidia kwa siku moja moja kwenye majengo hayo ili fedha walizopewa wazitumie na kuzimaliza ili waweze kuomba nyingine.

Katika hatua nyingine, halmashauri hiyo imepokea Sh. milioni 200 kwa ajili ya kuboresha kituo cha afya cha Rungwa na wananchi wameanza kujitolea nguvu kazi kwa kuchota maji, kuchota mchanga na ufyatuaji wa matofali.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo shule saba za msingi ndizo zilizopatiwa fedha Sh. milioni 75 na endapo zitatumika kwenye matundu ya vyoo zitapata matundu bora yatakayosaidia afya za watoto kuboreka.

# CRDB yatoa chakula cha Eid kwa watoto yatima

**Na Neema Hussein, KATAVI**

BENKI ya CRDB tawi la Mpanda mkoani Katavi, Iimetoa msaada wa chakula kwa watoto yatima wa dini ya Kiislam wanaoishi kwenye Manispaa ya Mpanda kwaajili ya Sikukuu ya Eid.

Akikabidhi msaada huo jana kwa Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Meneja wa CRDB tawi hilo, Hamad Masoud, alisema watoto hao wana haki ya kufurahia sikukuu kama walivyo watoto wengine ambao wana wazazi wao.

Masoud aliwataka watoto hao kutokujiona hawana thamani katika dunia, na kuwataka wasome kwa bidii huku wakiondoa fikra hizo kwa kuwa kuna watu wana historia kubwa katika maisha yao na sasa ni watu wakubwa hapa duniani.

"Yawezekana ukawa unajiona upo katika mazingira magumu sana, yawezekana ukawa umekata tamaa sana, yawezekana ukajiona wewe hapa duniani hufai, lakini mimi niwatie moyo na mjuwe kuwa Mwenyezi Mungu ndiyo mtoa riziki," alisema Masoud.

Shekhe Mkuu wa Mkoa, Mashaka Kakulukulu, aliishukuru benki hiyo kwa kufanya tukio hilo muhimu la kuwakusanya watoto na kuwapa zawadi kwaajili ya Eid kama vitabu vya dini vinavyo elekeza.

Alisema hiyo iwe ni ishara kwa Taasisi zingine au mtu mmoja mmoja kuiga mfano huo uliofanywa na benki hiyo na kujua kwamba wanao wajibu wa kuwalea watoto hao kwa sababu hawakupenda kuondokewa na wazazi wao.

Watoto waliopewa msaada huo pia walitoa shukrani zao kwa benki hiyo na uongozi wa Bakwata kwa kuwajali na kuwakumbuka katika kipindi cha Sikukuu ya Eid na kuomba waendelee kuwasaidia na kuwalea katika mazingira ya dini.

# Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kuua kwa kukusudia

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

MAHAKAMA Kuu Tanzania, Kanda ya Kigoma imemhukumu Semburi Mussa (45), kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua Luiza Gervas kwa kukusudia kwa kumcharanga mapanga kichwani na shingoni na kumsababishia kifo kinyume cha sheria.

Hukumu hiyo ilitolewa Mei 20, na Msajili wa Mahakama hiyo, Anord Kilekiano ambaye amepewa mamlaka ya kusikiliza kesi za Mahakama Kuu.

Msajili Kilekiano alisema ametoa hukumu hiyo ya kunyongwa hadi kufa baada ya upande wa mashitaka kuthibitisha kosa la mauaji ya kukusudia dhidi ya mshitakiwa huyo pasipokuacha shaka yoyote.

Alisema Mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshitakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na vijana wengine wenye tabia ya kikatili kama yake.

Alisema upande wa mashitaka ulipeleka mahakamani mashahidi sita na vielelezo viwili ambavyo vilithibitisha kuwa mshitakiwa huyo alimuua Luiza kwa kukusudia.

Upande wa mashitaka ulikuwa ukiongozwa na mawakili wawili wa serikali ambao ni Robert Magige na Raymond Kimbe na upande wa utetezi ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa kujitegemea, Abdulheri Hamadi, ambaye alikuwa akimtetea mshitakiwa.

Msajili huyo alisema shahidi wa kwanza upande wa mashitaka alidai mahakamani kuwa siku ya tukio alimuona marehemu akiwa anatoka shambani akiwa ameshika panga mkononi na mshitakiwa akiwa na fimbo mkononi na walipokutana njiani katika Kijiji cha Kaparamsenga ndipo mshitakiwa akamnyang'anya panga na kuanza kumkatakata sehemu za kichwani na shingoni ambaye alianguka na kuvuja damu nyingi.

Alisema watu walipiga kelele zilizosababisha askari mgambo kusaidia kumkamata mshitakiwa huyo na kumpeleka kambi ya jeshi iliyopo katika Kijiji cha Kaparamsenga.

Kadhalika, alisema Luiza alipelekwa katika Kituo cha afya cha Kijiji cha Kaparamsenga na kuthibitishwa kuwa alifariki dunia baada ya kuvuja damu nyingi.

Alisema mshitakiwa ni shemeji wa marehemu ambao walikuwa na ugomvi baada ya mke wa marehemu kupewa eneo ambalo marehemu alijenga nyumba katika eneo hilo.

Alisema kitendo hicho kilijenga chuki dhidi ya marehemu na mshitakiwa kwa kupewa eneo la mirathi, sababu alimuoa dada wa mshitakiwa.



Kaimu Meneja wa Wakala wa Vipimo Mkoa wa Shinyanga, Hilolimus Mahundi (kushoto), akionyesha moja kati ya mizani 27, mkoani humo juzi, ambazo wamezitaifisha kutoka kwa wafanyabiashara wilayani Kahama, kutokana na kutokidhi vigezo vya kuuzwa hapa nchini kutokana na kutengenezwa mahususi kwa ajili ya kuwaibia wananchi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Afariki dunia kwa kupondwa na lori

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

MKAZI wa Kijiji cha Uwanja wa Ndege, wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, Emmanuel Ligombaji (22), amefariki dunia baada ya kupondwa na lori.

Mashuhuda wa tukio hilo walisema kuwa ajali hiyo ilitokea katika eneo la Mlimamoyo baada ya lori hilo aina ya Scania lenye namba za usajili T 586 AGB, kushindwa kupanda na kurudi nyuma.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Ligombaji ambaye alikuwa mfanyakazi wake aliruka ili kuweka gogo kwa lengo la kulinusuru lisiendelee kurudi nyuma na kupinduka.

Walisema akiwa katika harakati hizo, alifanikiwa kuweka gogo hilo, lakini kwa bahati mbaya lori hilo ambalo lilikuwa kwenye mwendokasi lilirudi nyuma na kulipanda gogo hilo na kumkanyaga.

Mganga aliyeufanyia uchunguzi mwili wa marehemu, Dk. Steven Hokororo, alisema chanzo cha kifo hicho kilitokana na kutokwa na damu nyingi.

Dk. Hokororo alisema marehemu alipasuka tumbo, mbavu na kichwa baada kukanyagwa na lori hilo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo ambalo alisema lilitokea Mei 20 na kuongeza kuwa polisi wanaendelea na uchunguzi wa chanzo cha kifo hicho.

# RC amsimamisha kazi M/kiti BMU tuhuma za ubadhirifu

**Na Said Hamdani, KILWA MASOKO**

MKUU wa Wilaya ya Kilwa, Christopher Nubiagai, amemsimamisha kazi Mwenyekiti wa Hifadhi ya Bahari (BMU), Kata ya Masoko, Athumani Kimbendu, ili kupisha uchunguzi kwa tuhuma mbalimbali zinazomkabili zikiwamo ubadhirifu wa fedha za makusanyo ya ushuru.

Uamuzi huo ameuchukua kufuatia malalamiko kutoka kwa wananchi, wakiwamo wavuvi na wachuuzi wa mazao ya Bahari (samaki), wakati wa kikao cha kusikiliza kero na changamoto zinazoikabili jamii.

Shutuma zilizowasilishwa kwa kiongozi huyo ni kutosoma mapato na matumizi kwa wananchi na kutafuna fedha zitokanazo ukusanyaji ushuru wa Sh. milioni 1.5.

Madai mengine ni kutotoa stakabadhi kwa wavuvi na wachuuzi wa mazao ya bahari na kutosoma kwa wananchi mapato na matumizi yanatokana na ushuru wanaolipa kila siku.

Wakiwasilisha madai hayo mbele ya Mkuu huyo wa wilaya, kwa niaba ya wenzao, mvuvi Said Mussa, alidai kuanzia Mei 11, mwaka huu, BMU chini ya uongozi wa mwenyekiti Kimbendu, imeshindwa kukusanya angalau Sh. milioni 1.5, licha ya wavuvi na wachuuzi kulipa ushuru wanaotozwa.

Alisema hakuna mvuvi au mchuuzi wa Samaki anaekosa kulipa ushuru,lakini kinachowasikitisha zaidi hakuna taarifa ya mapato na matumizi wanayosomewa na pale wanapohoji utokea mtafaruku kati yao na uongozi wao wa BMU.

Mohamedi Msusa alidai kushuka kwa mapato yanayotokana na ushuru inachangiwa zaidi na mwenyekiti wao amekuwa ni mtu wa dili, ikiwemo kukusanya ushuru bila ya kutoa Stakabadhi kwa wachuuzi.

"Leo nawaelezeni ndugu zangu, huyu mwenyekiti ni mtu wa dili, ameshawahi kuchukuwa Sh. 20,000 kutoka chombo cha Kanali bila kutoa Stakabadhi na mimi kunipatia Sh.3,000 kuniziba mdomo" Alisema Mussa.

Pia alidai kulingana na uwepo mdogo wa maelewano kati yao na uongozi wa BMU Kata ya Masoko amemuomba Mkuu wa Wilaya hiyo ya Kilwa, Ngubiagai kusimamia hali hiyo kwa mustakabali ya Maendeleo ya wananchi wa Wilaya hiyo, Mkoa na Taifa kwa ujumla.

Mwenyekiti Kimbendu akijitetea mbele ya kikao hicho, alidai kushuka kwa mapato kunachangiwa zaidi na wavuvi kuuza mazao ya Bahari nyakati za usiku na Katibu wake kutowajibika ipasavyo katika ukusanyaji ushuru.

Akitangaza uwamuzi wake, Ngubiagai alisema kufuatia jamii kuchoshwa na kutotendewa haki, ikizingatia wapo tayari kulipa kodi na tozo zingine amemsimamisha kazi mwenyekiti huyo wa (BMU) ili kupisha uchunguzi na pale akionekana hana hatia atarejea kuendelea katika nafasi yake.

"Kufuatia tuhuma nyingi zinazomkabili, kuanzia leo ninamsimamisha kazi mwenyekiti wenu kupisha uchunguzi, ukionekana huna hatia utarejea na ukionekana upo ukweli, utalazimika kufikishwa kwenye vyombo vya Sheria", Alisema Ngubiagai.

Ngubiagai alisema kwa upande wao waajiri wao ni wananchi, ndio wanaowatumikia na si vinginevyo, hivyo kama hawezi ni bora kuachia mambo yakienda mrama.

# DC aagiza aliyeuza nyumba ya yatima akamatwe

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, ameliagiza Jeshi la Polisi, kumkamata Zakina Saidi, popote alipo na kumfikisha katika ofisi yake kwa tuhuma za kuuza nyumba ya urithi.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kuuza nyumba hiyo baada ya kukabidhiwa usimamizi wa mirathi ya watoto yatima Shamila Husseni na Omar Husseni.

Katambi, alitoa agizo hilo jijini hapa mara baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa watoto hao waliodai kuwa nyumba yao imeuzwa na shangazi yao.

Alisema kuwa kitendo hicho ofisi yake haitakifumbia macho cha kupora mali ya wanyonge.

"Huyu mama ambaye ni shangazi yao lazima jeshi la polisi mtafute na kumkamata aletwe ofisini kwangu kwa kuwa nimeshaagiza yeye pamoja na mnunuzi Aloyce Matambula, waje ofisini kwangu wanakaidi na hatimaye nyumba hii imeuzwa na hii notisi yake ni batili," alisema Katambi.

Alisema kuwa hukumu ambayo ilitolewa na Mahakama ya kumkabidhi usimamizi wa mirathi Zakia, ina upungufu mkubwa hivyo yeye kama msimamizi wa haki atahakikisha kuwa anaandika barua ya kuchambua na kuipeleka kwa Jaji wa Mahakama.

"Huwezi kuwa msimamizi wa mirathi, lakini pia uwe mmliki wa nyumba hiyo, huu ni uhuni hivyo basi nitoe rai kwa watu kama hawa ambao wanaishi kwa ujanja ujanja wa kutaka kutumia mali za yatima kujinufaisha badala ya kufanya kazi waache mara moja hatutawafumbia macho kabisa lazima tuwafunge akatulimie maharage,"alisema Katambi.

Awali, mmoja wa watoto hao Shamila, alisema wao ndiyo wamiliki halali kutokana na baba yao kuandika majina yao katika hati miliki halisi ya nyumba hiyo.

Alisema nyumba hiyo ndiyo walikuwa wanaitegemea yeye pamoja na mdogo wake kwa ajili ya kujipatia fedha za kujikimu.

"Nyumba hii tumepangisha wapangaji na tumekuwa tukijipatia fedha kutokana na kuweka wapangaji, lakini sasa wiki iliyopita tumeletewa notisi ya kutaka tuondoke ndani ya siku 14, kwa kuwa imeuzwa bila sisi kushirikishwa,"alisema.

Alisema baba yao alifariki miaka 21, iliyopita na shangazi yao hakuwahi kujitokeza, lakini wanashangaa ameibuka hivi karibuni na kudai yeye ndiye msimazi wa mirathi na kuuza nyumba hiyo kimyakimya kwa Sh. Milioni 45.



Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa, Raymond Mwangwala, akifungua jiwe la msingi wa ujenzi wa nyumba ya umoja huo, wilayani Bahi, mkoani Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## UVCCM kumchukulia fomu Magufuli

**Na Peter Mkwavila, BAHI**

UMOJA wa wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), umetangaza kumchukulia fomu ya kugombea urais, Rais John Magufuli katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu wa UVCCM Taifa, Raymond Mwangwala, alipokuwa akizungumza na vijana wa Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma kwenye uwekaji wa jiwe la msingi wa ujenzi wa nyumba ya vijana.

Aliwataka vijana wote nchini na Watanzania kuunga mkono azma yao kwa kumchangia na kumchukulia fomu hiyo kutokana na kufanya mapinduzi makubwa ya kiuchumi.

Alisema kila mtu ni shahidi kwa maendeleo anayoyaona na wamenufaika nayo, hivyo waendelee kumuunga mkono na kumpa ridhaa kuendelea na kipindi chake cha pili cha uongozi.

Akizungumzia uwekaji jiwe la msingi la ujenzi huo, Katibu huyo aliwapongeza vijana hao kwa ujenzi huo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa UVCCM, Wilaya ya Bahi, Hassani Kidoke, alisema ujenzi huo umefanikishwa baada ya vijana kutumia nguvu yao na kupewa msaada na wadau kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi.

Naye, Katibu wa UVCCM wilayani humo, Shabani Idd, alisema hadi kukamilika kwa ujenzi wa nyumba hiyo utagharimu Sh. milioni 22.

# Serikali yataja mikakati mitano usafiri majini

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

IKIWA ni miaka 24 tangu kutokea kwa ajali ya Mv. Bukoba, serikali imetaja mikakati mitano iliyochukuliwa ili kuimarisha usalama katika usafiri wa majini nchini.

Ajali hiyo ilitokea Mei 21, mwaka 1996, watu takribani 800 walipoteza maisha katika Ziwa Victoria na meli hiyo ilikuwa ikitokea Bukoba kwenda Mwanza na kuzama maeneo ya Bwiru.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alisema serikali imeboresha usafiri kwa njia ya maji katika maziwa makuu kwa kufanya miradi mbalimbali.

Alitaja miradi hiyo kuwa ni ukarabati wa meli mbili katika Ziwa Victoria ambazo ni Mv. Victoria na Mv. Butiama, ujenzi wa chelezo na ujenzi wa meli mpya kubwa katika Bandari ya Mwanza Kusini.

"Kwa kuwa tumekarabati meli na kujenga mpya katika ziwa lile lile iliyotokea ajali ya Mv. Bukoba, nimeona leo niwajulishe wananchi jinsi serikali ilivyojipanga kuhakikisha inarejesha usafiri katika ziwa hili,"alisema.

Vile vile, alisema tangu kutokea kwa ajali hiyo serikali imejizatiti na kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha usalama wa usafiri wa majini.

Alisema mkakati mwingine ni uboreshwaji wa Sheria na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Majini huku ikiimarisha usimamizi wa usalama wa usafiri majini kwa kuweka Ofisi na wakaguzi wa meli wa Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (Tasac) kwenye mikoa yote inayopakana na maziwa makuu.

"Ukaguzi huu unahakikisha kuwa meli zote zinazofanya safari majini zina vifaa vya kujiokolea vinavyotosheleza idadi ya watu waliomo kwenye chombo na abiria kupewa maelekezo ya kutumia vifaa hivyo," alisema.

Waziri Kamwelwe alitaja mkakati wa tatu ni kuboresha shughuli za utafutaji na uokoaji na kuanzisha kituo cha uokoaji na utafutaji cha Dar es Salaam.

"Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Bahari Duniani (IMO), imejenga kituo cha kuratibu shughuli za utafutaji na uokoaji katika Bandari ya Dar es Salaam na kinasimamiwa na Tasac, kinafanya kazi saa 24 na siku saba za wiki," alisema.

Akizungumzia mkakati wa nne wa miundombinu ya bandari, Kamwelwe alisema serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya Bandari katika Maziwa Makuu na Bahari ya Hindi ili kuwa salama na zenye ufanisi zaidi.

"Mkakati wa tano ni uboreshaji wa mafunzo na utoaji wa vyeti vya mabaharia, serikali imeimarisha usimamizi wake chini ya Chuo cha Bahari Dar es salaam (DMI), kwa mujibu wa Itifaki ya Kimataifa na vyeti vinatambuliwa kimataifa na mabaharia wa Tanzania watafanya kazi meli yoyote duniani,"alisema.

# Wawakilishi waomba kuvua barakoa wanapochangia

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

UVAAJI wa barakoa unawatesa baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kuwalazimu kuomba ruhusa kutoka kwa Spika wa Baraza hilo kuzivua wakati wakiwa wanazungumza katika kikao hicho.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, alilazimika kuvua barakoa wakati akisoma makadirio ya bajeti ya Wizara ya Uwezeshaji Wanawake na Watoto katika kikao cha Baraza la Wawakilishi baada ya kupata usumbufu ikiwamo kushindwa kupumua vizuri.

Waziri huyo alilazimika kuomba ruhusa ya kuvua barakoa kutoka kwa Spika wa Baraza hilo na kukubaliwa ombi lake.

"Mheshimiwa Spika naomba uniruhusu nivue barakoa kwa sababu kadri ninavyozungumza napata shida ya kupumua na hivyo kushindwa kuzungumza kwa ufanisi mkubwa," alisema.

Mwakilishi wa Jimbo la Ole, Mussa Ali Mussa, naye alilazimika kuomba ruhusa kutoka kwa Spika kuvua barakoa kutokana na kupata shida ya kuzungumza na kupumua.

Mussa alikuwa akichangia bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2020-2021 ambaye alizungumzia suala la ujenzi wa madarasa mapya katika shule za jimbo lake.

"Mheshimiwa Spika napata matatizo ya kuzungumza kutokana na utu uzima wangu hata pumzi zangu napumua kwa shida kutokana na barakoa kwa hivyo naomba kuivua ili nichangiye vizuri," alisema Mussa na kukubaliwa.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imewataka watu wote wanaoingia katika majengo ya serikali na kupata huduma ikiwamo wafanyakazi wake kuhakikisha wanavaa barakoa ikiwa ni moja ya hatua ya kujilinda na ugonjwa wa corona.



Waziri wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Muhammed (kulia), akijadiliana jambo na Mwakilishi wa Jimbo la Chukwani, Mwanaasha Khamis, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Shule kongwe za kihistoria kukarabatiwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar,imesema imejipanga kuzifanyia ukarabati mkubwa shule kongwe za kihistoria ziliopo eneo la Mji Mkongwe wa Zanzibar kwa lengo la kuimarisha sekta ya elimu.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020-2021.

Alizitaja shule zitakazofanyiwa ukarabati ni Benbella ambayo kwa sasa inachukua wanafunzi wa kike pekee na shule ya Haille Sellasia ambayo ilijengwa katika kipindi cha utawala wa kisultani.

Shule nyingine inayotarajiwa kufanyiwa ukarabati mkubwa ni ya Paje Mtule iliyopo Mkoa wa Kusini Unguja ambayo ujenzi wake ulikumbwa na kasoro mbalimbali.

Vile vile, aliitaja shule ya Chwaka Tumbe iliyopo Pemba kuwa ni miongoni mwa shule zitakazofanyiwa ukarabati ili ziweze kurudi katika hadhi yake na kuchukua idadi kubwa ya wanafunzi.

Alisema jumla ya shule 20 zitafanyiwa ukarabati wa kawaida kwa ajili ya kuruhusu kupokea wanafunzi wengi zaidi kwa wakati mmoja, kufuatia kujitokeza kwa tatizo la upungufu wa madarasa.

"Mheshimiwa Spika tumejipanga kuzifanyia ukarabati mkubwa shule kongwe zilizojengwa kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo zilitoa mchango mkubwa wa elimu kwa wanafunzi mbalimbali huku tukijipanga pia kuzifanyia ukarabati shule nyingine 20 za Unguja na Pemba," alisema.

Pembe alisema Wizara ya Elimu ipo katika hatua za mwisho za kuanza kwa ujenzi wa shule tatu za kisasa ambazo ni ufadhili kutoka Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA).

Alisema kuwa shule hizo zitajengwa huko Gamba na Mfenesini, Mkoa wa Kaskazini Unguja pamoja na Kifundo huko Pemba zikiwa za ghorofa.

Alisema kazi inayotarajiwa kufanywa kwa sasa ni kutangaza zabuni ya kutafuta mshauri mwelekezi atakayefanya kazi ya kusanifu michoro kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi wa shule hizo.

Pembe alichukua nafasi hiyo kuipongeza BADEA kwa msaada wake ambao ni sehemu ya kutekeleza ahadi zake za kuimarisha sekta ya elimu nchini.

"Mheshimiwa Spika nachukua nafasi hii kuipongeza BADEA kwa kutimiza ahadi yake ya kujenga shule tatu zenye hadhi ya ghorofa ambazo zitasaidia kupunguza tatizo la uhaba wa nafasi kwa wanafunzi wetu," alisema.

Pembe aliliomba Baraza la Wawakilishi kuidhinisha jumla ya Sh. 138,145,584,000 kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020-2021.

# Wanafunzi 30 waliopata ujauzito warejea shuleni

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SHERIA ya kuwalinda wari na mtoto wa mzazi mmoja Na.4 ya mwaka 2005 imewawezesha jumla ya wanafunzi 30 waliopata ujauzito kuendelea na masomo yao Unguja na Pemba kuanzia mwaka 2005-2015.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pemba Juma alisema hayo wakati akiwasilisha makadirio mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020-2021.

Alisema sheria hiyo imeleta mabadiliko makubwa ni mkombozi kwa watoto wa kike waliopata matatizo ya ujauzito, na kutoa nafasi ya kuwarudisha shule na kuendelea na masomo.

Alisema wapo wanafunzi waliopata ujauzito na kufaidika na sheria hiyo waliokubali kurudi shule na kuendelea na masomo na wapo waliofaulu hadi kidato cha sita na kuendelea vyuo vikuu.

Alisema jumla ya kesi za ndoa 13 zimeripotiwa katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kwa mujibu wa Sheria ya Elimu ya mwaka 1982 kifungu 20 (3), wanafunzi hao walifukuzwa shule kwa sababu wapo katika elimu ya lazima.

"Mheshimiwa Spika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, itaendelea kutekeleza Sheria ya wanafunzi wanaopata ujauzito kuendelea na shule ambayo tumeibaini kuleta mabadiliko makubwa ya maendeleo ya wanafunzi hao," alisema.

Pia, Pembe alisema Wizara ya Elimu imejipanga kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia vikiwamo vya kuwadhalilisha wanafunzi wa kike.

Aliwataka walimu kuhakikisha wanafuata maadili na kujiepusha na vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo kuwapa mimba wanafunzi wa kike.

"Matukio ya walimu kuwapa mimba wanafunzi yamepungua sana kwa sababu sasa wanajifahamu na kuyajua majukumu yao kama ni walezi wa wanafunzi wanapokuwa katika maeneo ya shule," alisema.

Alisema Wizara ya Elimu ipo katika mchakato wa rasimu ya sheria ya elimu ambayo tayari imepelekwa kwa wadau kwa ajili ya kujadiliwa.



**SHAY USILIE, MWACHIE MUNGU ATAWAADHIBU** Uk. 14

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI MEI 23, 2020



## KINARA

# Idriss aongoza mastaa walioonja rumande

MSANII wa Vichekesho nchini, Idriss Sultan, wiki hii imekuwa mbaya kwake, baada ya kujikuta akiswekwa rumande kutokana na kudaiwa kwenda kinyume na sheria ya makosa ya mtandao.

Sultan ambaye alikuwa mshindi wa shindano la Big Brother Africa, alikamatwa mwanzoni mwa wiki baada ya kutakiwa kuripoti kituo cha polisi cha Oysterbay jijini Dar es Salaam.

Msanii huyo amekuwa na wakati mgumu kutokana na kukumbana na matukio mengi ya kukamatwa kuliko wengine, jambo ambalo mashabiki wake wanaamini kutokana na vichekesho vyake kuwa na utata.

Pengine Sultani anakuwa msanii wa kwanza kuitwa na kuhojiwa mara nyingi na polisi kutokana na kazi zake kuibua hisia tofauti.

Mara ya kwanza, alikamatwa baada ya kutoa posti ya kumpongeza Rais Dk. John Magufuli, siku yake ya kuzaliwa ambayo iliambatana na picha aliyohariri na kuleta maoni mchanganyiko.

Tukio la pili ni lile la kukamatwa na kufunguliwa kesi ambayo anadaiwa kuweka maudhui kwenye mtandao ambao haukusajiliwa na Mamlaka ya mawasiliano nchini. Hii sasa ni mara ya tatu kuwekwa rumande kwa madai kukiuka sheria ya mtandao ambayo haijakuwa wazi.

Wakili wa mchekeshaji huyo, amesema msanii huyo bado anahojiwa na polisi kutokana na kukiuka sheria hiyo .

Kwa mujibu wa wakili Benedict Ishabakaki, amesema polisi walifanya upekuzi nyumbani kwa mteja wake.

"Tunataraji anaweza kuachiwa kwa dhamana...masharti tuliyopewa ni awe na wadhamini wawili wanaotambuliwa na serikali ya mtaa," amesema wakili Ishabakaki.

Kutokana na matukio hayo, baadhi ya mashabiki wake wamempa ushauri wa kujirafakari wapi anakosea ili kulinda kipaji chake.

"Idriss Sultan ni msanii mzuri, lakini hili la kukamatwa kila siku linaleta picha tofauti, akitoka lazima ajitafakari ili kujiepusha na mambo haya," aliandika Juma Saidi.

BASI SAWA

## Waziri Shonza kumbe kanogewa 'Kaka Tuchati'

NAIBU Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza, ametangaza kuwa mfuasi wa ngoma mpya ya kundi la Rostam inayoitwa "kaka tuchati".

Akizungumza kwa njia ya simu kupitia show ya "Friday Night Live", Shonza amesema hayo wakati akielezea namna alivyotoa ushauri kwa wanamitindo Callisah na Ben Breaker, ambao walikuwa wana bifu kwa muda mrefu.

"Niwapongeze kwa kuwakutanisha hao vijana wetu wawili, nafikiri sisi kama Wizara ambayo tunasimamia kazi za sanaa naona tasnia ya ubunifu na uwanamitindo bado ni changa hapa kwetu na inakua, kwa hiyo waliokuwapo wanahitaji kuunganisha nguvu ya pamoja ndiyo maana nikawasisitiza huu sio wakati wa malumbano na kuangalia nani mkubwa nani mdogo" ameeleza Waziri Shonza.



## Ibraah hukujua kutafuta kazi?

MWIMBAJI wa Bongo Fleva anayekuja kwa kasi, Ibraah Tz, amesimulia jinsi alivyohangaika kukutana na Harmonize, hadi sasa kipaji chake kiameanza kuonekana.

"Kabla ya kukutana na Harmonize, nilikuwa naenda sana getini kwake kuomba nafasi ya kuonana naye kwa miezi miwili, lakini sikupata nafasi hiyo, ila kuna mjomba wangu alikuwa ananisadia kunipa nauli, akajitahidi kunikutanisha na producer Bonga, hatimaye nikapata nafasi ya kufika Konde Music" ameeleza Ibraah

Ibraah Tz ameendelea kusema kabla hajasainiwa Konde Gang, amezunguka sana kwenye studio mbalimbali kutafuta msaada, hata hivyo ilishindikana.






## Duh! We Calissah akisikia Wema utampandisha shetani

MWANAMITINDO maarufu nchini, Calisah, amesema mwigizaji wa Bongo Muvi, Wema Sepetu, hapindui kwake na hata akitaka kwenda kwake hawezi kumzuia.

Akizungumza na EATV, Calisah amesema yeye na msanii huyo wana uhusiano mzuri na mara kadhaa wanaongea na kujadiliana mambo mbalimbali ya maisha.

"Wema ndiyo mtu ninayewasiliana naye sana, haipiti siku mbili tunaongea na hapa kuna meseji zake, sijui nikuonyeshe...Lakini nitaonekana nam-snitch kwa sababu vitaleta picha mbaya na siwezi kuonyesha kila kitu hatuna matatizo yoyote".



## 20 percent kuendeleza 'Furaha Iko Wapi?'

MWANAMUZIKI mkongwe wa Bongo-Fleva, 20 Percent, amesema filamu ya 'Furaha Iko Wapi' na wimbo wa Mama Neema, ni kisa cha kweli japo haimuhusu moja kwa moja.

Akizungumza katika kipindi cha PlanetBongo cha East Africa Radio, msanii huyo ameeleza kuwa, Neema yupo hadi leo nchini Rwanda na kwamba anakuja na filamu nyingine inayoendeleza kisa hicho.

"Ile ngoma ya Mama Neema ni stori ya ukweli japo hainihusu mimi moja kwa moja, Neema sasa hivi ni mkubwa na anajiheshimu kama Monalisa, japo kwa sasa yupo nchini Rwanda. Binafsi nimebarikiwa kupata watoto wa kutosha yaani ninao wengi" amesema 20 Percent.

## Wazazi walioimba na watoto wao




**Na Adam Fungamwango**

HUKO nyuma tulikuwa tunaona tu kwenye nchi za wenzetu, baba na mwanaye au ndugu wa damu wanapiga muziki katika bendi moja.

Mfano kundi la Jackson Five, lilikokuwa na Michael Jackson na ndugu zake, hadi pale alipojitenga na kila mtu kuimba kivyake.

Hapa Tanzania kuna baadhi ya wanamuziki ambao walifanya kazi hiyo na baadaye watoto wao wakaja kurithi. Mbali na hilo watoto hao wakaja kuimba tena na wazazi wao.

Hawa wafuatano ni baadhi ya wazazi na watoto zao ambao waliimba kwa pamoja.

**NGUZA VIKING NA PAPY KOCHA**

Nguza Viking ni mpiga solo maarufu nchini aliyekuwa akiliongoza kundi zima la Maquiz Du Zaire, baadaye ikaja kuwa Maquiz Original. Baadaye aliunda kundi lake la Achigo Band na kuanza pia kuimba.

Mtoto wake Papy Nguza baadaye naye akaja kuwa mwanamuziki, akipigia bendi za TOT Plus, FM Academia na zingine.

Hatimaye aliungana na baba yake na kuimba pamoja wimbo ya 'Seya' uliojipatia umaarufu mkubwa.

**ZAHIR ALLY ZORRO NA BANANA ZORRO**

Zahir ni mwimbaji na mtunzi aliyepigia bendi mbalimbali, ikiwamo JKT Mafinga maarufu kama Kimulimuli, Sambulumaa na nyingine nyingi.

Baada ya kijana wake Banana Zorro akaja kuwa mwanamuziki. Akaungana na baba yake kuimba na kutoa vibao mbalimbali ikiwemo 'Nzela' ambao ulitingisha sana ulipotoka.

**MAX BUSHOKE NA RUTA BUSHOKE**

Max, alikuwa ni mwimbaji na mtunzi mahiri wa bendi ya DDC Mlimani Park Orchestra.

Aliimba na kutunga vibao vingi kama 'Visa Vya Mesenja' na vingine vingi.

Baada ya miaka kadhaa, mtoto wake wa kiume, Ruta naye akaja kuwa mwimbaji wa bongo fleva.

Naye baadaye alikuja kuimba na baba yake waliporudia baadhi ya vibao vya DDC Mlimani Park.

**TX MOSHI WILLIAM NA TX JUNIOR**

Marehemu Tx Moshi William ni mwanamuziki anayekumbukwa kwa uwezo wake mkubwa wa kutunga na kuimba nyimbo zilizopendwa na kuwa maarufu sana akiwa na bendi ya Juwata Jazz, au Msondo Ngoma Music Band.

Mwanamuziki huyo kabla hajafariki mwaka 2006, kijana wake Hassan Moshi alikuwa tayari ameshaanza kujifunza muziki.

Ingawa hakuimba naye kwenye bendi ya Msondo ambayo Hassan kwa sasa yupo, lakini wameshiriki wote kwenye baadhi ya nyimbo chake kwenye bendi ya Zing Zong inayoitwa Bana Mwambe.

**HADIJA KOPA NA ZUCHU**

Malkia wa Mipasho Afrika Mashariki, Hadija Kopa ni mmoja wa waimba taarabu maarufu zaidi Ukanda wa Afrika Mashariki. Alianzia muziki wake Zanzibar na baadaye akajiunga na kundi la TOT Taarabu ambalo ndiyo kwa kiasi kikubwa lilimpa sifa.

Ana binti yake anaitwa Zuchu ambaye naye sasa amekuwa mwimbaji. Binti huyu anaimba bongo fleva na nyimbo zenye mahadhi ya mduara.

Naye ameungana na mama yake kutoa ngoma moja kali ya mahadhi ya Pwani iitwayo 'Mauzauza' ambayo imebamba kinoma kwa mashabiki wa muziki Bongo.

## Fumanizi: Hujui thamani ya mkia mpaka ukatwe

**Na Adam Fungamwango**

MNYAMA yoyote huwa hajui thamani ya mkia wake, hadi pale unapokatwa. Hivyo hivyo kwa binadamu, anaweza asijue thamani ya kitu alichonacho hadi pale anapokuwa hana.

Filamu ya 'Fumanizi' imeeleza kila kitu kinachoonyesha kuwa thamani ya kitu hutokea pale tu mtu anapokikosa.

Said, kijana aliyekuwa na mke mwema, anakubaliana na mpango wa baba yake mzee Korongo kutaka kuoa mke wa pili.

Baba anamtaka kijana wake kuoa na mke mwingine, lakini akitaka amuoe binti mmoja mrembo Saida kwa sababu amempenda sana binti huyo anayelelewa na Bi. Mwenda.

Harusi imefanyika, lakini mke wa pili alipokanyaga tu nyumbani, mke wa kwanza Husna akawa hana thamani tena kwa Said.

Kazi ni kumpiga kila kukicha na hatimaye kumtimua nyumbani. Pamoja na kumfukuza, lakini hakumpa talaka. Jaffar akamchukua dada yake na kumpeleka kwa mjumbe ili ampe hifadhi.

Pamoja na kukaa kwa mjumbe, lakini vikao vya mara kwa mara vilikuwa vinafanyika, ili Said amrudie mkewe, au kama hamtaki, basi ampe talaka kwa sababu kwa hapati huduma kutoka kwa mume au mtu yoyote yule.

Maisha ya Said na mkewe wa pili, yanakuwa kama ya tamthilia. Mke hapiki, hapakui, hafui.

Yeye kutwa na simu tu kuchati. Said ndiyo anafua, anaosha vyombo, anapika 'dada', yaani ilikuwa ni kama yeye ndiye ameolewa.

Hakuna marefu yasiyo na ncha. Sijui dawa 'zilieksipaya' mwaya? Basi ndoa ikaanza kuingia mushkeli, Said kageuka, akaanza kumkumbuka mkewe.

Siku hiyo kaenda kwa mjumbe, kufika huko hali aliyomuona nayo, akaanguka na kuzirai.

Mama wee, kamkuta mkewe kitumbo ndii. Ukaanza msako nani kampa nani mimba.

Kumbe ni kijana mmoja karibu na nyuma ya mjumbe. Kijana Gimbi alichukulia udhaifu wa Said.

Mwanamama alihitaji faraja, matunzo na mtu wa kumpetipeti. Yote akayapata kwa Gimbi.

Mume katafakari, mwisho anaona kosa ni lake. Hakuna aliyemuadhibu Gimbi kwa hilo.

Akaamua kumchukua mkewe Husna hivyo hivyo pamoja na mimba. Akasema ataitunza, ili mradi tu yeye anamtaka mkewe Husna.

Wazee wakamwambia kuwa kwa sababu mke alikuwa hana miezi mitatu tangu aondoke nyumbani, lakini pia hajampa talaka mkewe, basi kiumbe kilichopo tumbani kihalali kinahesabika kuwa ni cha mume.

Said akamchukua mkewe Husna na kumrudisha nyumbani.





# Boyce, mpenzi wake wakutwa wamefariki

STAA Gregory Boyce, ambaye anajulikana kama Tyler Crowley, amekutwa amefariki yeye na mpenzi wake Natalie Adepoju, ndani ya chumba chake.

Boyce amekutwa amefariki siku ya jumanne pamoja na mpenzi wake huyo raia wa Nigeria, katika nyumba yake iliyopo Las Vegas.

"Mpwa wa Greg alipoamka aliona gari la mjomba wake bado lipo nyumbani, alikuwa na wasiwasi kwa sababu wakati huo alitakiwa kuwa Los Angeles. Alipokwenda alimkuta yupo ndani," alisema repota wa EOnline.



## Shay usilie, mwachie Mungu

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Seyi Shay, amelalamika akaunti yake ya Instagram, imezuiliwa na kudukuliwa na watu wasiojulikana.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, Shay amesema kwa sasa hawezi kufanya chochote katika akaunti yake hiyo kutokana na watu hao kufunga kila kitu.


"Siwezi kusema chochote wala kufanya jambo kutokana na Instagram yangu kuzuiliwa na mambo yangu ya siri yapo hatarini," amesema Shay.

## Medikal kweli au fiksi zako?

RAPA kutoka Ghana, Sebastian Marroquin, maarufu kama 'Medikal', ameibua majadala mkali katika mitandao ya kijamii, baada ya kudai amealikwa na mtoto wa muuza dawa za kulevya tajiri duniani, Pablo Escobar.

Medikal, alianza kuwashangaza watu baada ya kuandika ujumbe kwenye ukurasa wake wa Twitter kuwa anasubiri muda wa kwenda kukuna na Juan Pablo Escobar, ambaye ni mtoto wa pekee wa Escobar aliyefariki mwaka 1993.

Ujumbe huo uliwapa mashaka mashabiki wake, lakini mwanamuziki huyo aliweka hadharani picha za ujumbe wa Juan ukisema ""Karibu Colombia, nijulishe unaposafiri ili nihakikishe kama unahudumiwa kwa upendo".






## Kolawole kumbuka una mke staa

MUME wa mwigizaji, Toyin Abraham, amefanya mashabiki wake kumwagia sifa baada ya kutoka na mtindo mpya wa nywele.

Kolawole Ajeyemi, ambaye anasifika kutokana na tabia yake ya umaridadi, ameweka video fupi katika ukurasa wake wa Instagram, akionekana akiwa tofauti na muonekano wa nyuma.

Kitendo cha kubadili ukataji wa nywele zake, ilisababisha baadhi ya mashabiki wake hasa wa kike kumwagia sifa kutokana na kutoka bomba.

## Lilian ya kale ni dhahabu

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Lilian Esoro, amewapa ushauri mashabiki wake, akiwaambia waache kuangalia uhusiano uliopita na badala yake wasonge mbele.

Lilian amewataka mashabiki wake wanawake kupiga hatua, wasihangaike kumuuliza kuhusu mume wake wa zamani Ubi Franklin, kwani kila kitu kwao kimeisha.

Esoro na mfanyabiashara Franklin, walioana na kudumu kwenye ndoa kwa mwaka mmoja na kisha waliachana.



MAKALA



Miradi ya uchimbaji wa kisima inayotekelezwa na FFWP vijijini

# FFWP inavyopambana na umasikini Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

VITA dhidi ya umasikini ni mapambano yanayohitaji nguvu kuishinda kutoka maeneo mbalimbali, kuanzia serikali, taasisi binafsi na mwananchi mmoja mmoja.

Katika kupambana na adui umasikini, baadhi ya mashirika yamekuwa na mchango mkubwa katika kusaidia jamii kujikomboa kiuchumi.

Moja ya wadau wanaopambana kuhakikisha umasikini unatoweka hapa nchini, ni Shirika linalofahamika Familia kwa Amani ya Dunia (FFWP). Asasi hii inalenga kugusa jamii na kueneza amani duniani kuanzia kwenye hatua ya kifamilia.

FFWP imekuwa ikitoa elimu ya maadili mema kwa wanafamilia kuanzia malezi ya watoto, uhusiano kwa wanandoa na wajibu wa wazazi kwa watoto.

Pamoja na wajibu wake wa kutoa elimu kwa familia, taasisi imekuwa ikitoa misaada mbalimbali katika maeneo kadhaa.

Akizungumza wakati alipotembelea Kituo cha Habari dhidi ya Umasikini (MeCAP), Mkurugenzi wa FFWP, Stylos Simbabwene, amesema kwamba Shirika lake limejikita kusaidia kwenye baadhi ya huduma za jamii kwa nia ya kupunguza umasikini kwa vitendo.

Simbamwene, anasema shirika lake limesaidia mradi wa uwekaji wa mfumo wa maji safi na ukarabati wa kisima cha maji katika Kituo cha Polisi Sitakishari wilayani Ilala jijini Dar es Salaam.

Lakini katika kituo hicho, FFWP wamegharamia uwekaji wa umeme katika jengo la Dawati la Jinsia ili wananchi wapate huduma bora na katika mazingira mazuri.

Vituo vingine vilivyonufaika na mradi huo ni Manzese na Kigogo Luhanga.

Anasema kwamba wamekarabati kisima cha maji katika Shule ya Msingi Mji Mpya wilayani Ilala na ukarabati wa lifti kwenye uwanja wa Taifa.

"Katika mradi huu wa kuboresha sehemu za kutolea huduma, tumejenga jengo la ofisi za serikali ya mtaa wa Msigani wilayani Ubungo, na Temeke tumechangia vifaa katika ujenzi wa ofisi ya CCM Azimio" amesema Simbamwene.

Mkurugenzi huyo anaeleza shirika hilo sio tu limetoa misaada katika Jiji la Dar es Salaam, pia wamesaidia baadhi ya miradi katika mikoa mingine.

"Tunafanya kazi zetu nchi nzima. Tumechangia ujenzi wa zahanati ya Engutoto wilayani Arumeru mkoani Arusha lakini pia uchimbaji wa visima wilayani humo", anaongeza kusema Simbamwene.

"Katika wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro, Shirika letu limejenga zahanati, kuchimba kisima cha maji na ununuzi wa gari la wagonjwa katika kijiji cha Manza".anazidi kufafanua

Mkurugenzi huyo anaeleza katika mkoa wa Mbeya, wamechimba kisima cha maji katika Shule ya Msingi Mwaheki na kuwezesha vikundi mbalimbali vya ujasiriamali.

Simbamwene amevitaja baadhi ya vikundi ambavyo Shirika lake limeviwezesha kuwa ni pamoja na kikundi cha ushonaji Majohe, kikundi cha kinamama Mvuti , vikundi vya Vicoba vya Kinyerezi, Kinondoni, Kigogo, Malamba Mawili na Mtoni kwa Aziz Ally, vyote vya jijini Dar es Salaam.

Amevitaja vikundi vingine kuwa ni kikundi cha Vicoba Arumeru mkoani Arusha, kikundi cha Vicoba Muungano mkoani Mbeya pamoja na mradi wa kinamama wa vyakula vya mifugo wilayani Arumeru.

"Pamoja na haya yote FFWP ni taasisi ya kwanza kuvunja rekodi ya uchangiaji wa damu nyingi zaidi katika hospitali ya taifa ya Muhimbili, Benki ya Damu na Hospitali ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI:.

Mkurugenzi huyo amesema kwamba Shirika lake limefanya kazi kubwa ya kutoa elimu ya maadili katika mikoa mbalimbali.

Ameitaja mikoa ambayo Shirika hilo limeshatoa elimu katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Mbeya, Arusha, Manyara, Singida, Pwani na Njombe.

"Katika elimu tumetoa udhamini ama ufadhili kwa viongozi wa makundi mbalimbali kuhudhuria mikutano au semina za kimaendeleo katika nchi mbalimbali" amesema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa MeCAP, Mdoe Kiligo, amelipongeza Shirika hilo kwa kuwapunguzia wananchi wengi mzigo wa umasikini wanaokabiliana nao.

"Kwa mfano tunapoambiwa FFWP, wamechimba visima katika maeneo ambako huduma ya maji safi na salama ilikuwa tatizo, wamesaidia sio tu kuwapatia wananchi huduma hiyo, lakini pia kuokoa muda ambao wananchi hao walikuwa wanautumia kutafuta maji, ili kufanya shughuli nyingine za uzalishaji mali. Hawa ni marafiki wa kweli katika mapambano dhidi ya adui umasikini".



Uchangiaji wa damu ni sehemu ya kampeni inayofanywa na FFWP katika kuboresha afya ya wananchi nchini

# Mchango kusajili jina la biashara katika kujenga soko la ushindani

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA biashara, ushindani ni vigumu sana kuuepuka, hii ni kwa sababu katika biashara yeyote mtu atakayoanzisha ni lazima kuna watangulizi au kuna wengine ambao watakuja baada ya kupendezwa nayo.

Kwa mjasiriamali au mfanyabiashara yeyote ni vyema kufahamu bayana kwamba ili biashara ikue ni lazima wigo wake katika soko uongezeke kwa kadri muda unavyokwenda.

Wigo wa soko hupimwa kwa kuangalia biashara inayotoa huduma au kuuza bidhaa zake kwa kiwango kikubwa kushinda zingine za namna moja.

Mfano kama soko la uuzaji maji ni asilimia mia moja na Wafanyabiashara katika soko hilo wapo watatu yani A, B na C.

Mfanyabiashara A. ameshika soko kwa asilimia arobaini huku wafanyabiashara B na C wakishika kwa asilimia thelathini kila moja, basi kwa hatma hii mfanyabiashara A ndiye anafanya vizuri zaidi.

Makala hii itaangazia mikakati kadhaa ambayo mfanyabiashara anaweza kuitumia ili kuweza kujiongezea nafasi katika soko la bidhaa anayouza au huduma anayotoa.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Brela, Godfrey Nyaisa

**Ubunifu**

Mmoja kati ya wataalam wa masuala ya masoko duniani, Leslie Kramer, anaeleza kwamba ili mfanyabiashara apate nafasi katika soko ni lazima awe mbunifu katika njia za kufikisha bidhaa au huduma yake kwa wateja wapya.

Ubunifu huu pia ni kutumia mbinu katika biashara yake ambazo hazijawahi kutumiwa na wapinzani katika soko hilo.

**Kuimarisha uhusiano na wateja**

Siri moja ya biashara ni kuhakikisha idadi ya wateja haipungui, mfanyabiashara mzuri hujenga uhusiano mzuri na wateja wake ili wasije kuhamia kwa mfanyabiashara mwingine.

Wahenga walisema mteja ni mfalme, anapenda siku zote kusikilizwa na kupewa huduma ya kumridhisha.

Hivyo mfanyabiashara unatakiwa kujenga uhusiano mzuri na wateja kwa kuwasikiliza na kufanyia kazi maoni yao, jitihada hizi zinatakiwa ziende sambamba na kuvutia wateja wapya.

Kwa kufanya hivi tarajia matokeo mawili, moja ni kuwalinda wateja wa biashara yako na mbili utavutia wateja wapya kila siku hivyo biashara itaendelea kukua siku hadi siku.

**Tengeneza mkakati wa kuongeza wigo wa soko**

Mkakati huu unasimamia vitu viwili vikuu, moja ni malengo na mbili ni muda wa kuyafikia hayo malengo. Unaweza kuwa wa mwaka mmoja na ukagawa utekelezaji wake kwa awamu nne, kila awamu ikiwa na miezi mitatu.

Mkakati huu utasaidia kupima na kufahamu kama malengo uliyoweka kutekeleza ndani ya kila awamu umefanikiwa au hapana na kujua sababu hasa ni zipi.

**Kuipatia jina biashara yako**

Jina la biashara ni utambulisho wa biashara fulani, Jina hili huipatia biashara uwezo wa kutambulika na kukumbukwa na wateja katika namna mbalimbali.

Wateja wanaweza kuitambua biashara yako kwa kutajiwa jina pekee hata kama hawajawahi kufika lakini pia wanaweza kuitambua biashara kwa kuelekezwa na watu wengine na wakafika sehemu ilipo biashara hiyo.

Jina la biashara pia ni muhimu kwa ajili ya kuitangaza biashara yako kupitia njia mbalimbali na watu wakaifikia kwa urahisi.

Ni muhimu pia kuzingatia kwamba sifa kuu ya Jina la biashara ni upekee, haitakiwi kufanana jina la mtu mwingine, kwa sababu hii itawachanganya wateja wanaotaka huduma.

Mara baada ya kupata Jina la biashara, namna nzuri ya kulinda upekee ni kufanya usajili katika Mamlaka husika ili kupewa haki ya kutumia jina hilo katika biashara peke yako.

Kwa Tanzania mamlaka inayohusika na usajili wa jina la biashara ni Wakala ya Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ambayo inatoa huduma hii kwa njia ya mtandao.

Meneja Uhusiano wa (BRELA) Robetha Makinda, anasema kigezo pekee kwa ajili ya kusajili jina la biashara ni kuwa na namba ya utambulisho wa Taifa kutoka NIDA.

Anasema anayehitaji kusajili jina la biashara atatakiwa kufungua akaunti katika nfumo wa usajili kwa njia ya Mtandao ya (ORS), hivyo atatembelea tovuti ya www.brela.go.tz .

Aidha, anasema baada ya kufungua akaunti atatakiwa kuandaa ombi lenye taarifa zake za biashara na kutuma BRELA ambapo atalipia kiasi cha Sh. 20,000/- pekee.

Kisha atapata cheti ambacho kinampatia haki ya umiliki wa jina hilo la biashara.

"Wahenga walisema "mtoto umleavyo ndivyo akuavyo" kwa muktadha huu biashara ni kama mtoto, njia ambazo zinatumika kuilea biashara ndizo zitakazo ifanya ikue, idumae au ifilisike." anasema.



Elimu inatumika katika kuhamasisha watu kusajili jina la biashara kwa kutumia mtandao

# Mawaziri 10 Sudan Kusini wakutwa na virusi corona

**JUBA,** Sudan Kusini

JUMLA ya mawaziri 10 wa Sudan Kusini, wamewekwa katika karantini baada ya kukutwa wameambukizwa virusi vya corona,

Waziri wa Habari wa nchi hiyo, Michael Makuei, alisema jana kuwa mawaziri hao wote walikuwa wajumbe wa kamati ya serikali ya kupambana na corona.

Mjumbe pekee katika kamati hiyo ambaye hakupatikana na virusi vya corona ni Waziri wa Afya, ambaye anaendelea na majukumu yake.

**Mpaka sasa zaidi ya watu 300 wamethibitishwa kupata corona, sita wamefariki dunia na wengine wanne wamepona.**

Ilielezwa kuwa viongozi hao wamepata maambukizo baada ya kukutana na aliyekuwa mjumbe wa kamati hiyo ambaye alikuwa na virusi hivyo.

Makuei, alisema mawaziri wote wanaendelea vizuri kiafya.

Siku chache zilizopita, Makamu wa Kwanza wa Rais wa nchi hiyo, Riek Machar na mkewe, ambaye ni Waziri wa Ulinzi, walijitangaza kuwa wamekutwa na virusi vya corona.

Hata hivyo, baadhi ya askari wanaowalinda viongozi kadhaa nchini humo wamekutwa na virusi na kuwekwa karantini.

Mpaka sasa zaidi ya watu 300 wamethibitishwa kupata corona, sita wamefariki dunia na wengine wanne wamepona.

Kwa upande mwingine, Umoja wa Mataifa umetoa tahadhari kuhusu hatari ya kuanguka kwa mfumo wa afya wa nchi hiyo ambayo ina uwezo mdogo wa kiuchumi baada ya kuathirika na vita kwa muda mrefu. **BBC**



Mwendesha pikipiki katika mji wa Satkhira, Bangladesh, akiangalia sehemu ya kupita baada ya kimbunga Amphan kuangusha mti na kuzuia barabara. **PICHA: REUTERS**

# Wafanyakazi wa afya 10,000 Iran waambukizwa corona

**TEHRAN,** Iran

WAFANYAKAZI 10,000 wa sekta ya afya nchini Iran, wameathirika na Covid-19, wakati wakitekeleza majukumu yao ya kazi.

Naibu Waziri wa Afya wa nchi hiyo, Qassem Janbabaei, alinukuliwa na vyombo vya habari jana akisema, hata hivyo hakufafanua kwa undani kuhusu jambo hilo.

Katika ripoti zilizotolewa hivi karibuni, serikali ya nchi hiyo ilitoa idadi ya wafanyakazi wa huduma ya afya walioambukizwa virusi hivyo ni 800 pekee. Iran imesema zaidi ya watu 100 miongoni mwao wakiwa wafanyakazi hao wamefariki.

Iran imekuwa taifa la Mashariki ya Kati linalokabiliwa na mlipuko mbaya zaidi wa virusi vya corona, takriban watu 7,249 wamepoteza maisha kati ya watu 129,000 waliothibitishwa kuambukizwa.

Hata hivyo, Shirika la Afya Duniani, WHO, limeonya kuwa makadirio yake yanaonyesha kwamba, nusu ya idadi ya watu wa Yemen wanaofikia milioni 30 wanaweza kuambukizwa virusi vya corona.

Katika makadirio hayo, watu 40,000 wanaweza kupoteza maisha kama hatua za haraka hazitachukuliwa kuwalinda raia hao wanaondelea kushuhudia vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Shirika hilo pia limeelezea wasiwasi wake virusi hivyo kusambaa eneo la Ukanda wa Gaza, baada ya Wizara ya Afya ya Palestina kuripoti visa vipya 35 katika siku tatu zilizopita, na kuifanya idadi kuwa na wagonjwa 55. **DW**

## Trump aamrisha bendera kupepea nusu mlingoti

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ameagiza bendera zipepee nusu mlingoti kwa ajili ya kuwakumbuka maelfu ya watu waliofariki kutokana na ugonjwa wa corona,

Kiongozi huyo, aliandika ujumbe kwenye ukurasa wake wa Twitter, akisema amri hiyo utalenga ofisi zote za serikali na itadumu kwa muda wa siku tatu.

Alisema hatua hiyi inalenga kuwakumbuka Wamarekani waliopoteza maisha katika janga la virusi vya corona.

Trump alifanya ziara katika kiwanda cha magari ya Ford, na katika hali ya kushangaza hakuvaa mavazi ya kujikinga, licha ya mwanasheria wa jimbo la Michigan kumuomba kufanya hivyo. **DW**

## Kenya yatabiri ongezeko wagonjwa corona

**NAIROBI,** Kenya

KENYA imetoa tahadhari kwa wananchi wake kujiandaa kushuhudia idadi kubwa ya wagonjwa wa corona kwa miezi mitano ijayo.

Wizara ya Afya nchini hiyo, imesema idadi hiyo ya juu ya visa vya maambukizo ya Covid-19 itafikia kilele chake mwezi Agosti na Septemba.

"Tunatabiri kwamba kilele cha ugonjwa huu nchini kwetu, kitakuwa miezi ya Agosti hadi Septemba, tutakuwa tunarekodi waathirika karibu watu 200 kwa siku, endapo tutaendelea kuchukua na hatua tulizoanza kuzitekeleza" alisema Mkurugenzi wa Afya ya Umma, Patrick Amoth.

Katika mpango huo, serikali ya nchi hiyo imepanga kuanza kupima watu zaidi ya 3,000 kwa siku baada ya kuwa na vifaa vya kutosha vya kupima virusi vya corona ambavyo vinaweza kutumika kwa muda wa mwezi mmoja.

Waziri wa Afya, Mutahi Kagwe (pichani chini), siku ya Alhamisi, alisema jumla ya watu waliopata virusi vya corona ilifikia 1,109, wakati 80 walikuwa wapya baada ya kupimwa kwa sampuli 3,102.

"Kadiri tutakavyopima watu zaidi, ndivyo tutakavyofahamu virusi hivi vimesambaa kwa kiwango gani." Alisema Kagwe. **BBC**



## China yashutumiwa sheria kuidhibiti Hong Kong

**BEIJING,** China

CHINA imeshutumiwa kutokana na hatua yake ya kulazimisha sheria ya usalama katika kisiwa cha Hong Kong.

Wanaharakati wanaotetea uhuru wa mji huo, wametishia kuingia mitaani kuandamana kupinga sheria inayopendekezwa, ambayo inatarajiwa kupiga marufuku vitendo vya uhaini, mapinduzi na uchochezi.

Sheria hiyo iliwasilishwa kwenye bunge la China mwanzoni mwa kikao chake cha kila mwaka, kilichofanyika jana asubuhi.

Awali viongozi wa kikomunisti wa China, walionya hawatavumilia uasi mjini Hong Kong, ambao una mamlaka yake ya ndani.

Mwaka jana, mji huo ulikumbwa na maandamano makubwa ya kuteteta demokrasia kwa siku saba mfululizo. **DW**

# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote, afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

## Mauaji Harusini- 17

Mtunzi anapatikana (0716 350534)




**Na Adam Fungamwangwo**

"Usilie. Msichana mdogo, mzuri na mrembo kama wewe hupaswi kulia hapa. Angalia watu waliopita njiani wanakuangalia unavyolia. Mimi mwenyewe nimeumia kutokana na kifo cha shangazi yangu, lakini silii. Mungu anasema umuombe huku na wewe unafanya kazi. Kazi itakayofuata sasa ni kuwasaka wauaji."

Maneno hayo yaliendelea kumshangaza na kumshtusha Shani. Aliwaza kuwa huenda anaongea na mtu wa kawaida "Au mzimu, maana huku ni makaburini?" Alijisemea mwenyewe.

Kwa mbali akaanza kumuogopa. Lakini hakuweza kujiondoa kwenye kifua chake kwa sababu ambazo hata mwenyewe hakuzifahamu.

"Uwasake wauaji, kwani unawajua?"

"Siwajui?"

"Sasa utawasaka vipi?"

Eddy aliachia tabasamu pana la kujiamini. "Hakuna yoyote atakayefanya kitu chochote duniani kwa siri kikakosa kujulikana."

Shani alizidi kupatwa na mshangao juu ya kijana yule aliyekutana naye makaburini. Pamoja na utanashati wake, lakini alionekana ni mtu anayejiamini "Kingine nini vile?" Alijiuliza. Lakini hakupata jibu.

"Kwani wewe unaitwa nani?" Shani kwa mara ya kwanza naye alimuuliza.

"Naitwa Eddy Kamal"

"Ni askari wewe kwani."

**Sikiliza Paul sisi siyo watoto. Sumu tutakayoitafuta si ya mamba wala ya kulia panya. Tutatafuta sumu ambayo inaweza kuingia kwenye mwili wa biandamu na kumuua baada ya miezi miwili au mitatu. Na kazi hiyo ya kuisaka niachieni mimi.**

"Hapana, mimi nilikwambia mwanzo nimetoka kusoma Marekani. Kwa sasa sina kazi yoyote ile."

"Uko nyumbani tu?"

"Ndiyo maana yake."

Kwa kipindi kifupi tu, Shani alitokea kumuamini na kupenda staili za kijana huyu mwenye tabia ya kujiamini.

"Nadhani sasa tuondoke." Eddy alimwambia.

Kwa shida Shani alijipapatua kwenye kifua cha Eddy na kuanza kutembea taratibu.

Alikuwa akijishangaa awali alikuja akiwa na nguvu, lakini kwa sasa ni kama ameishiwa nguvu, huku akionekana kujidekeza zaidi. "Sababu ni nini?" Alijiuliza. Hakupata jibu.

Hatua chache mbele, gari aina ya Land Cruiser nyeusi ilikuwa imeegeshwa. Na ndipo hatua za Shani zilipokomea.

"Nikushukuru rafiki yangu Kamal. Kwa muda mfupi tu tumekutana hapa makaburini, lakini umenipa kampani ya kutosha. Mimi narudi nyumbani, naomba namba zako, nitakutafuta siku nyingine ili tuongee zaidi, maana naona kama vile sisi ni ndugu." Shani alisema huku akimpa mkono wa kwaheri Eddy.

Wakati huo Shani alikuwa anafungua mlango wa gari hilo. Eddy hakushangaa sana kwa sababu tangu yupo nchini Marekani alisikia kuwa mjomba wake aliyemuoa shangazi yake Patiyo alikuwa tajiri mkubwa.

"Usihofu mtoto wa shangazi yangu, nitajie wewe namba zako, halafu nitapiga ili wewe upate za kwangu na mimi za kwako. Nadhani kila mtu akipata za mwenzake itakuwa vema zaidi."

Shani akafanya kama alivyoambiwa. Baada ya Shani kuondoka, aliliendea gari lake Toyota Brevis, naye taratibu akaanza kukata mitaa ya Kinondoni makaburini akirejea kwake Kijitonyama.

***************************

Kwenye ukumbi mmoja maeneo ya Magomeni Mikumi, mkutano wa pili wa ndugu wa marehemu Patiyo ulifanyika tena kwa siri.

Lengo ni lile lile ni kutaka kumtoa duniani Shani, ili mradi tu ndugu hao warithi mali za ndugu yao huyo.

Kwa wao Shani ilikuwa ni kikwazo cha kuipata mali ya mamilioni ya ndugu yao, ambayo aliichuma kwa jasho, kabla ya kuuawa na watu wasiojulikana masaa machache baada ya kufunga ndoa na mkewe Grace.

Patiyo aliacha mtoto mmoja tu wa kike, Shani ambaye kihalali ndiyo mrithi.

Uchu wa mali uliwashika wanandugu hao na wakaungana, wakiwa na nia moja thabiti ya kuhakikisha binti yule mdogo mwenye miaka 23 tu apoteze maisha.

"Tumefikia wapi?" Jim, ambaye ni mkubwa wa kuzaliwa aliuliza.

"Kaka ulisema kila mtu aje na mpango mkakati wake, mimi nimekuja na wazo." Paul, ambaye ni wa mwisho kuzaliwa kwenye familia ya marehemu Patiyo alimwagika.

"Enhee tueleze."

"Mimi nadhani tungekodisha gari aina ya lori ambalo limvizie na kugongana naye uso kwa uso na kumuua. Wapo watu wa aina hiyo na ni wataalamu, wao kumgonga akiwa na gari lake la fahari ni kazi ndogo tu na kila mmoja atadhani ni ajali ya kawaida tu," alisema Paul.

"Sawa wazo lako si baya, limefika, ngoja tuulize na wengine." Jim alisema huku akiwageukia ndugu zake wengine. "George na wewe?"

"Kama mimi wazo langu ni kwamba, katika uchunguzi wangu mdogo nimegundua kuwa hupenda kwenda kula chakula cha mchana ABC Club kila Jumamosi, sasa cha kufanya ni kufanya kila njia, kumtafuta mtu pale ili afanya kazi moja tu. Ya kumuwekea sumu ili imuue." George aliwasilisha mchango wake.

'Ahsante kwa mchango mzuri, ndugu yangu Ben wewe nawe unasemaje?" Jim alimgeukia ndugu yake mwingine Ben.

"Mimi bwana wazo langu ni kwamba tutafute watu wamfuatilie akiwa na gari lake, akishuka wamateke, halafu wamepeleke wakaojua wao halafu wamuue, hapo tatizo litakuwa limemalizika na mali yote ya ndugu yetu Patiyo itakuwa mikononi mwetu." alisema Ben.

"Michango yenu leo yote ni mizuri. Mimi pia kama kaka yenu nilikuwa na mchango wangu, lakini kuna mchango mmoja hapa nauona utatufaa sana.

Ndugu wote watatu, Ben, George na Paul walimtazana kaka yao Jim kwa makini.

"Mchango wa Geogre naona unafaa sana. Amesema kila Jumamosi huwa anakwenda kwenye Club moja maarufu ya ABC iko kule Mbezi Beach, imechangamka kweli kweli, yeye huwa anakwenda kula chakula cha mchana. Sasa hapa cha kufanya ni kitu kimoja tu. Tumtafute mfanyakazi mmoja wa hiyo hoteli sijui Club, tena awe mpishi. Tumpe pesa ya maana afanye kazi ndogo tu," alisema Jim na kuwaangalia akiwakazia macho wenzake.

"Amuwekee sumu kwenye chakula chake tu ambacho ameagiza. Na sumu hiyo tuitafute sisi wenyewe. Wakati tunampa pesa ya awali mtu huyo, apewe na hiyo sumu kwa ajili ya kumunyunyuzia." Kama mkubwa Jim alisema akiwaangalia wenzake, lakini kwa sasa tabasamu lilionekana dhahiri usoni mwake.

"Kaka wewe si unaijua sumu?" Paul aliuliza.

"Yaani awekewe sumu kwenye chakula, si ataanguka na kufa hapo hapo hata hajamaliza na poli wakija kazi ya kwanza watakayoifanya ni kuwazoa wafanyakazi wote na hamuoni kuwa adhabu kidogo tu watakayopewa, mmoja wapo atasema ni yeye ndiye aliyeweka sumu na akatutaja sisi?" Paul alionyesha wasiwasi na mpango huo.

"Sikiliza Paul sisi siyo watoto. Sumu tutakayoitafuta si ya mamba wala ya kulia panya. Tutatafuta sumu ambayo inaweza kuingia kwenye mwili wa biandamu na kumuua baada ya miezi miwili au mitatu. Na kazi hiyo ya kuisaka niachieni mimi." Jim alijinadi na kuwashangaza ndugu zake kwa akili kubwa na maarifa aliyokuwa nayo.

Mpango ukawa umekamilika. Kila mmoja akawa ameridhishwa na mpango ule.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Malundi Kija Malundi** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **SANLG** yenye namba za usajili **T58 BJM.** Injini namba **No. SLJ 57FMJ.**

**Chessis No. *LBRSPJBS0A9013228.**
Hivyo yeyote atakayeiona kadi hiyo atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi kilichopo Mjini Bariadi.

Taarifa ya kupotea kwa kadi hiyo, imetolewa katika kituo cha polisi cha Bariadi kwa namba: BAR/RB/3642/2011.

157491

### KUPOTEA KWA CHETI



**Catherine Jumanne Mavere anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne Kilichotolewa kwa mtahiniwa namba S.0250-0010 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kwa mtihani wa mwaka 2010 katika shule ya Sekondari Wasichana Murigha.**

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.**

**Taarifa ya polisi namba RV/RB/4073/2019.**

157490

### BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA

**SHAURI LA GHARAMA NA.93/2020**

**NATIONAL MICROFINANCE BANK::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::MDAI**

**DHIDI YA**

**VICTOR R.MWASHINGAIRE::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::MDAIWA**

**YAH : KUITWA SHAURINI**

KWA:
1.VICTOR R.MWASHINGAIRE
Fahamu kwamba National Microfinance Bank amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.

Shauri limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 26/05/2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.A.Mapunda Mwenyekiti wa Baraza. Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.

Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au muwakilishi ameruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya ya eneo la sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka:usipo hudhuria siku hiyo,baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 22/04/2020.

157492

### KUPOTEA KWA KADI

EZEKIA ELIAS TWEVE ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA **SANLG T 780 BKR** ILIYOTOLEWA NA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA.

YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

POLISI TAARIFA: **99108127441141**

157489

***Uza, Chenye***

***Thamani***

***Kubwa Kwa***

***Kutangaza***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

**Nipashe**
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# PJANIC YUKO NJIA PANDA JUVENTUS




**TURIN,** Italia

NYOTA wa Juventus, Miralem Pjanic amesema "majaliwa yake ya baadaye yanategemea na kile unachokifanya leo" huku uvumi ukizidi kukuwa akihusishwa na mabingwa wa LaLiga, Barcelona.

Pjanic amekuwa akihusishwa zaidi kuhusu tetesi za usajili wake, huku kiungo huyo akitajwa uhamisho wake kutoka kwa mabingwa hao wa Serie A kwenda Barca unaweza kumhusisha Arthur.

Paris Saint-Germain na Chelsea pia zimeripotiwa kumwania mchezaji huyo wa kimataifa wa Bosnia-Herzegovina.

Wakati Juve walirudi kwenye mazoezi wiki hii baada ya mlipuko wa virusi vya corona, Pjanic aliweka ujumbe wenye utata kwenye mtandao wa kijamii Alhamisi.

Pjanic aliandika: "Majaliwa ya baadaye yanategemeana na kile unachokifanya leo. Nafurahia kururi uwanjani."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 alijiunga na Juve akitokea kwa wapizani wao, Roma mwaka 2016.

Tangu atue pale Turin, Pjanic ameshinda mataji matatu mfululizo ya Serie A pamoja na Coppa Italia na Supercoppa Italiana.

# Silva aihofia Madrid Uefa

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester City, Bernardo Silva ameonya kuwa Real Madrid bado wana nafasi licha ya wao kuibuka na ushindi kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya 16 bora katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Miamba hao wa Ligi Kuu England waliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Madrid kwenye mchezo wa kwanza pale katika dimba la Santiago Bernabeu Februari mwaka huu.

Baada ya michezo kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, imeripotiwa kwamba michuano hiyo inaweza kurejea Agosti, mwaka huu.

Licha ya City kuwa kwenye nafasi nzuri, Silva anaihofia Madrid, ambayo ilishinda mara tatu mfululizo kati ya mara nne ya michuano hiyo iliyopita.

"Huwezi kuwaondoa kabisa Real Madrid ambao wameshinda mara 13 taji la Ulaya," alisema kiungo huyo akinukuliwa na gazeti la AS.

"Hakuna mwenye uzoefu kama ilivyo kwa wachezaji wa Madrid katika mashindano haya, hivyo tusifikiri kwamba tayari tumewafunga."

Silva aliongeza: "Bado nafasi ipo wazi. Wakati unapocheza na timu kama Madrid chochote kinaweza kutokea. Tumeona kwa misimu michache iliyopita walivyopambana."







# Capello amwonya Martinez kuhusu kutua Barcelona

**MILAN,** Italia

FABIO Capello amemsifia nyota wa Inter Milan, Lautaro Martinez, lakini amemwonya fowadi huyo kuwa ni bora kuanza kwenye Serie A kuliko kukaa benchi pale Barcelona.

Martinez amekuwa akihusishwa kuwaniwa na miamba hao wa LaLiga, akiwa amefunga mabao 16 katika mechi 31 za Inter msimu huu.

Huku Capello akiwa anavutiwa na kipaji cha nyota huyo wa kimataifa wa Argentina, kocha huyo wa zamani wa Real Madrid na Juventus amesema Martinez atakabiliwa na changamoto ya kupenya kwenye kikosi cha kwanza cha Barcelona.

"Lautaro Martinez ni mchezaji mzuri sana," amesema Capello akiliambia gazeti la El Larguero.

"Ana kila aina ya ubora, ana kasi na pia ni mzuri sana kwa kufunga mabao.

"Kwenda Barcelona na kuwa kwenye kikosi cha kwanza dhidi ya Luis Suarez itakuwa ngumu pale.

"Nafikiri ni bora angebakia katika kikosi cha Inter kuliko kwenda Barcelona na kuanzia benchi."

Martinez amefunga mabao 25 katika mechi 66 kwa Inter tangu alipowasili hapo akitokea Racing Club mwaka 2018.

# Vidal hana mpango wa kuondoka Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

KIUNGO wa Barcelona, Arturo Vidal, amesisitiza ana furaha zaidi hapo kwenye klabu hiyo ya LaLiga huku kukiwa na uvumi wa kuhusishwa kwenda Inter Milan.

Vidal mwenye umri wa miaka 32, ameripotiwa kuwaniwa na Inter, ambako ataungana na kocha wake wa zamani kule Juventus, Antonio Conte.

Lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Chile, ambaye mkataba wake pale Camp Nou unamalizika mwaka 2021, amesema ana furaha kuwapo hapo Barcelona.

"Nina furaha na nimetulia hapa Barcelona, bila shaka nataka kuendelea. Sasa nimejiandaa zaidi kuliko mwanzo," amesema Vidal wakati wa mahojiano live kupitia kwenye Instagram.

"Nina furaha, kuna kundi zuri na nina marafiki wakubwa kwenye vyumba vya kubadilishia nguo."

LaLiga inakaribia kurudi baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona tangu Machi.

Vidal amesema yupo tayari kuisaidia Barcelona kwenye mbio za ubingwa wa LaLiga ambapo





# RIVALDO AMSHAURI HAALAND AENDE REAL MADRID

**MADRID,** Hispania

RIVALDO anaamini Erling Haaland anaweza kung'ara zaidi kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, wakati Real Madrid wakimkodolea macho straika huyo wa Borussia Dortmund.

Haaland alijiunga na Dortmund kutoka Salzburg Januari, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 tayari amekuwa akihusishwa na miamba hao wa LaLiga, Madrid.

Raia huyo wa Norway amefunga mabao 10 kwenye Bundesliga katika mechi tisa alizocheza, na 13 kwenye mashindano yote kwa Dortmund.

Nyota wa zamani wa Barcelona, Rivaldo aliandika kwenye Betfair: "Tayari ni mchezaji mkubwa, lakini katika umri wa miaka 19 anaweza kuwa bora zaidi kwa siku zijazo na kuwa mmoja wa washambuliaji bora duniani.

"Na ana kila aina ya ubora, anacheza bila woga na ni mtulivu sana, ni aina ya mchezaji wa daraja la juu na anaweza kujifunza mengi.

"Tayari kuna watu wanafananisha staili ya uchezaji ya Haaland na Ronaldo Nazario na kunaweza kuwa na mfanano, kwani Haaland ana kasi na mwepesi wa kufunga, lakini ni mapema mno kufikiria kumlinganisha na Ronaldo.

"Real Madrid naona ndio sehemu inayomfaa Haaland na akitua pale ana uwezekano mkubwa wa kung'ara zaidi na kuwa katika daraja la juu."

# *Liverpool ipo tayari kwa ubingwa – Henderson*

**LIVERPOOL,** England

NAHODHA wa Liverpool, Jordan Henderson anajiamni kwamba vinara hao wa Ligi Kuu England wapo tayari kupambana uwanjani wakati ligi hiyo itakaporejea.

Vijana hao wa kocha, Jurgen Klopp, walikuwa wanaongoza kwa tofauti ya pointi 25 wakati ligi hiyo iliposimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona na sasa wanawania kutwaa taji lao la kwanza la ligi tangu mwaka 1990.

Ligi Kuu England inatarajiwa kurejea Juni mwaka huu na klabu zimeanza mazoezi mapema wiki hii.

Na Henderson anaamini kwamba, Liverpool wapo tayari kupambana uwanjani na kwamba ana uhakika watalibeba taji hilo.

Amesema: "Unahitaji kuendelea kuwa fiti kwa kiwango cha juu ili kuendelea kucheza vizuri dimbani," amesema akiiambia Sky Sport.

"Kwa sasa tumeanza mazoezi na tutarejea uwanjani hivi karibuni na tumeshajiandaa kwa ajili ya kubeba taji la Ligi Kuu."



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BARCA, TER STEGEN SASA WAKUBALIANA

## ●●● Vigogo hao wakamilisha mazungumzo na kumaliza ndoto za Bayern kunasa saini...

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona iko katika hatua za kusaini mkataba mpya na golikipa wake, Marc-Andre ter Stegen baada ya majadiliano waliyokuwa wanafanya kuelekea kwenye makubaliano, jarida la Sport limeeleza.

**Uamuzi huo utawafanya vigogo hao wa Hispania kumaliza tetesi za golikipa huyo chaguo la kwanza kutakiwa na mabingwa wa Bundesliga, klabu ya Bayern Munich.**

Gazeti moja la Hispania limeandika mazungumzo ya golikipa huyo na Barcelona yanaelekea mwishoni na wakati wowote atakamata kalamu na kusaini mkataba mpya ambao utamweka klabuni hapo hadi mwaka 2025.

Kwa sasa Ter Stegen analipwa mshahara wa pauni 140,000 kwa wiki lakini mshahara huo unatarajiwa kuongezeka baada ya kusaini mkataba mwingine wa kuendelea kubakia hapo Nou Camp.

Mlinda mlango huyo mwenye umri wa miaka 28 alijiunga na Barca mwaka 2014 akitokea Borussia Moenchengladbach na kwa sasa kiwango chake kimeimarika na kuwa mmoja wa wachezaji muhimu kwenye klabu hiyo.

Inaelezwa mwezi uliopita klabu hiyo inayoshiriki LaLiga ilikuwa na wakati mgumu kufikia makubaliano na wakala wa Ter Stegen, lakini Sport limeandika sasa wamefikia muafaka na kumaliza tofauti zilizokuwapo.

Machi, mwaka huu Bayern ilitajwa kuandaa dau la pauni milioni 90 ambalo lingeweka rekodi ya dunia ili kupata saini ya nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, ingawa sasa wanaonekana kupunguza kasi katika kukamilisha mchakato huo.

Mwezi uliopita, rafiki wa karibu wa mchezaji huyo alisema Ter Stegen anasisitiza anataka kubakia Kataluny na nafasi ya kwanza anaipa Barcelona.

Kwa sasa inaonekana tayari ameshafanya uamuzi wa kubakia klabuni hapo na kinachosubiriwa ni taratibu za kiutawala za kusaini mkataba huo mpya, Sport liliripoti.

Mkataba wa sasa wa golikipa huyo ambao dau lake la kuondoka klabuni hapo limetajwa kuwa ni pauni milioni 161, unatarajiwa kumalizika ifikapo majira ya joto mwaka 2022.

## ZISIKUPITE

### DAU LA UMTITI LAPUNGUA

BARCELONA imeamua kupungua bei ya beki wake Mfaransa Samuel Umtiti (26), na kuwa pauni milioni 27, licha ya kuwapo kwa tetesi za kutakiwa na Manchester United na Arsenal. ***(Sport - in Spanish)***

### UNITED, MADRID ZATULIZWA

REAL Madrid na Manchester United zitalazimika kusubiri miaka miwili ipite ili kumsajili straika wa Borussia Dortmund, Erling Haaland (19), kwa sababu mkataba wa nyota huyo kutoka Norway kuna kipengele kitakachomruhusu kuhama klabu hiyo kwa dau la euro milioni 75 itakapofika mwaka 2022. ***(Evening Standard)***

### AKANJI ANUKIA ARSENAL

ARSENAL inajipanga kumsajili beki wa Dortmund na Timu ya Taifa ya Uswisi, Manuel Akanji (24) kwa dau la pauni milioni 25, baada ya kuanza mazungumzo naye tangu Januari, mwaka huu. (Sun)

### PJANIC KUBAKIA JUVE

KIUNGO wa Juventus na Timu ya Taifa ya Bosnia-Herzegovina, Miralem Pjanic (30), anatarajia kukacha ofa ya kujiunga na Ligi Kuu England katika kipindi cha majira ya joto, Chelsea ni moja ya klabu zinazotajwa kuhitaji huduma yake. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### ARSENAL, EVERTON VITANI

ARSENAL imeungana na Everton katika mbio za kuwania saini ya kiungo wa Juventus Mfaransa Adrien Rabiot (25), na inaamini ikimsajili atatengeneza 'pacha' nzuri na Matteo Guendouzi (21). ***(Le10 Sport - in French)***

### TAGLIAFICO ATAJWA ARSENAL

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anataka kumsajili beki wa kushoto wa Ajax na Timu ya Taifa ya Argentina, Nicolas Tagliafico (27), ambaye thamani yake imetangazwa kuwa ni pauni milioni 20. ***(Sun)***

### CARLOS ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL imeweka wazi ina mpango wa kumsajili beki wa Sevilla Mbrazili Diego Carlos, ambaye ana umri wa miaka 27. ***(Marca - in Spanish)***

### ROSE AMTAJA RODGERS

BEKI wa Tottenham Hotspur, Danny Rose, ambaye kwa sasa yuko kwa Newcastle United ameweka wazi anataka kufanya kazi na Kocha wa Leicester City, Brendan Rodgers, lakini akitania angependa kuona Ben Chilwell (22), ananunuliwa kwanza. ***(Mail)***

### PSG, AUBAMEYANG BADO

PARIS St-Germain imeendelea kuwa kimya kuhusu uamuzi wa kumsajili mshambuliaji wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang (30), ambaye amebakiza mkataba wa mwaka mmoja kwenye klabu yake hiyo inayotumia Uwanja wa Emirates. ***(Le10 Sport - in French)***

### TODIBO KUTUA EVERTON

EVERTON inaongoza kwenye mbio za kuwania saini ya beki wa Barcelona, Jean-Clair Todibo. Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 20 alikuwa kwa mkopo wa mwaka mmoja katika klabu ya Schalke msimu huu. ***(Sport - in Spanish)***

HABARI MICHEZO

## Biashara United kuendeleza 'dozi'

Na Adam Fungamwango

WAKATI imefurahia uamuzi wa kurejesha Ligi Kuu Bara, uongozi wa Biashara United wamesema wamejipanga kusaka matokeo mazuri kama walivyokuwa wanashinda kabla ya ligi hiyo kusimamishwa kutokana na ugonjwa wa COVID-19.

Ofisa Habari wa Biashara United, Shomari Bhinda, alisema wameipokea taarifa ya Rais Dk. John Magufuli ya kufungua michezo kwa unyeyekevu na mikono mawili na tayari wamewaita wachezaji kwa ajili ya kuanza rasmi mazoezi ya pamoja.

"Kwanza tunampongeza Rais (JPM), kwa kuruhusu tena michezo, lakini sisi kama Biashara tumejipanga kisawasawa. Tumejipanga kuendeleza 'dozi' kama tulivyokuwa tukifanya kabla ya ligi haijasimamishwa. Si unajua kuwa wakati huo tulikuwa bora kabisa," alisema Bhinda.

Alisema kuwa wachezaji wao wote wako hapa nchini, ikiwamo wale wa kimataifa, hivyo wataingia uwanjani wakiwa na kikosi kilichokamilika.

Katika mechi tano za mwisho, Biashara United yenye pointi 40 na katika msimamo wa Ligi Kuu ikiwa kwenye nafasi ya 10, ilishinda mechi mbili, sare mbili na kufungwa moja.

## Kijangwani yaanza kujiimarisha Z'bar

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Kijangwani FC inayoshiriki Ligi Daraja la Pili Mkoa wa Mjini Magharibi, Aboubakar Waziri, amesema timu yake imeanza maandalizi ili kuhakikisha inafanya vema na kupanda daraja katika msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Waziri alisema kwa msimu huu wanajipanga kuhakikisha hawashuki daraja na nguvu 'mpya' wanaziandaa kwa ajili ya msimu mpya wa 2020/21.

Waziri alisema timu yake ilipoteza matumaini ya kupanda daraja baada ya mipango yao kuvurugika kwa kufanya vibaya katika michezo kadhaa iliyopita na 'kuzima' ndoto zao.

Alisema licha ya kikosi chake kuundwa na wachezaji wazuri na vijana lakini changamoto ya utawala ilisababisha kushindwa kufikia malengo waliyoyapanga kwenye msimu huu.

"Timu ina wachezaji wazuri, vijana na wanaendana na kasi ya ligi, ila naomba viongozi wetu wahakikishe msimu unaokuja wanatatua changamoto zinazoikabili timu hii, hususani mambo muhimu yanayopaswa kuwafikia wachezaji," Waziri alisema.

Kijangwani FC ipo katika nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Daraja la Pili Mkoa wa Mjini Magharibi yenye kushirikisha timu 14 na imebakiza mechi tatu ili kukamilisha msimu wa ligi hiyo.

# YANGA YAJIPANGA KURUDI 'KIVINGINE' LIGI KUU BARA

Na Shufaa Lyimo

KLABU ya Yanga ya jijini Dar es Salaam, imesema imejipanga kurejea vizuri na 'kivingine' katika Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inatarajiwa kuendelea tena kuanzia Juni, Mosi mwaka huu, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Mashindano wa Yanga, Thabit Kandoro, alisema kabla Rais John Pombe Magufuli hajatoa kauli ya kufungulia michezo, klabu yao ilikuwa imeshajipanga na tayari kuendeleza mapambano.

"Sisi kipindi chote ambacho Ligi Kuu ilikuwa imesimama, tulikuwa na mipango mingi ya kuhakikisha timu inaendelea kufanya mazoezi kama kawaida kwa kila mchezaji kufuata maelekezo yaliyotolewa na makocha wetu," alisema Kandoro.

**Kiongozi huyo alisema kipindi chote hicho makocha walikuwa wanafuatilia ratiba za kila mchezaji bila kujali yupo ndani au nje ya nchi na uamuzi huo ulisaidia kuwaimarisha na kuwaandaa kukabiliana na ushindani.**

"Tulikuwa tunatembelea kila mchezaji na kushuhudia wakati anajinoa, na kwale waliopo nje ya nchi tulikuwa tunawasiliana nao kwa njia ya video ili kupata uhakika wa kile wanachokifanya," Kandoro alisema.

Aliongeza wamejipanga kurudi uwanjani wakionyesha soka la ushindani ili malengo yao ya kumaliza kwenye nafasi za juu katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara yatimie.

"Tumefurahia taarifa za ligi, hatujashtushwa na habari hizo, kwa sababu muda wowote tulikuwa tunasubiri tamko hilo na wachezaji wote wapo fiti kurudi uwanjani kuendelea na michezo iliyobakia," alisema kiongozi huyo.

Yanga yenye pointi 51 iko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kucheza michezo 27.

Simba ndio mabingwa watetezi na vinara wa ligi hiyo inayoshirikisha klabu 20 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.



Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara (katikati), akiingia kwa mbembwe kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam huku akisindikizwa na mabaunsa wawili siku ya Tamasha la Simba Day mwaka jana. **PICHA : MAKTABA**

# Maproo wainyima usingizi Azam FC

Na Saada Akida

WAKATI kipenga cha kurejea kwa Ligi Kuu Tanzania Bara kimeshawaka, mabosi wa Azam FC 'wanaumia kichwa' kwa sababu ya kuwakosa wachezaji wake wa kimataifa saba ambao bado hawajarejea nchini, imeelezwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', aliliambia gazeti hili kukosekana kwa wachezaji hao wa kimataifa kutakuwa ni pengo kwa kikosi chao.

Popat alisema licha ya Tanzania kufungua anga yake, lakini nchi nyingine zikiwamo Ghana, Zimbabwe na Uganda bado hawajafungua mipaka na viwanja vyao vya ndege.

"Tumepata taarifa Ghana wanatarajia kufungua mipaka yao Juni 15, mwaka huu na huko kuna wachezaji wetu watatu (Razak Abalora, Yakub Mohammed na Daniel Amoah)," alisema Popat.

Aliwataja wachezaji wao wengine ambao hawako nchini ni pamoja na Mganda Nicholas Wadada, Never Tigere, Donald Ngoma na Bruce Kangwa walioko Zimbabwe.

"Leo (jana) Bodi ya Ligi na Wizara zilitarajia kukutana, tunasubiri taarifa kutoka kwao ikiwa ni kuanza rasmi Juni Mosi, kwetu itakuwa ni changamoto, sasa vichwa vinauma juu ya kuwakosa wachezaji wetu hawa lakini pia na makocha," alisema Popat.

Alisema Kocha Mkuu Arastica Cioaba alirejea kwao Romania huku msaidizi wake, Vivier Bahati ambaye ni raia wa Burundi pia alikwenda kwao.

"Inapofika kwa makocha hapo ni mtihani, maana walimu wetu wote kutoka nje, wawili kutoka Romania na mmoja Mrundi, yeye hapa Burundi tuna imani hakuna shida," Popat alisema.

Alimtaja mshambuliaji pekee aliyebakia ambaye ataongoza safu ya ushambuliaji ni Mzambia Obrey Chirwa.

Michezo
Jumamosi Mei 23, 2020
Nipashe



Barca, Ter Stegen sasa wakubaliana UKURASA 22



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, ambaye jana jijini Dodoma alitoa ufafanuzi kuhusiana na kurejea kwa Ligi Kuu Bara. **PICHA: MAKTABA**

# Ligi Kuu Bara sasa bila ya mashabiki

●●● Yapangwa kuchezwa katika vituo, Sh. milioni 417 zatengwa kwa ajili ya posho, malazi...

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetangaza kutenga kiasi cha Sh. milioni 417 kwa ajili ya kuziwezesha timu zinazoshiriki ligi mbalimbali nchini kumalizia msimu wa 2019/20 ambao ulisimama ili kujikinga na maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19), imefahamika.

**Akizungumza jijini hapa jana, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alisema wameamua kutoa fedha hizo ili kuzisaidia timu gharama za uendeshaji baada ya Rais Dk. John Pombe Magufuli kutangaza kufungua michezo hapa nchini.**

Mwakyembe alisema serikali kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na Bodi ya Ligi Nchini (TPLB), ziliona haitakuwa na tija kama wataziachа timu bila ya kuwasaidia katika kipindi hiki chenye changamoto.

"Kwa maana hii sasa, serikali kwa kushirikiana na Tff, Bodi ya Ligi pamoja na wadhamini, wameamua kutoa kiasi hichi cha fedha ili kuziwezesha timu hizi kumaliza mashindano na msimu wa mwaka 2019/20," alisema Mwakyembe.

Alisema wataanza na michezo ya Ligi Kuu Bara, Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili na mashindano ya Kombe la FA na ligi hizo zitachezwa katika vituo viwili vya Dar es Saalam na Mwanza ili kupunguza gharama za uendeshaji.

"Kiasi hichi cha fedha kitatumika katika kuziondolea gharama timu kama vile posho za wachezaji, malazi pamoja na chakula, hatutaki kusikia kuna timu imekosa chakula wakati ligi imeanza, ndio maana tumeondoa ule mfumo wa nyumbani na ugenini ili kupunguza gharama katika kipindi hicho cha corona," Mwakyembe alisema.

Alisema kituo cha Dar es Saalam kitahusisha mechi za Ligi Kuu na michuano ya Kombe la FA kwenye Uwanja wa Taifa, Azam Complex na Uhuru wakati Ligi Daraja la Kwanza na Ligi Daraja la Pili zitachezwa katika Uwanja wa CCM Kirumba na Nyamagana jijini Mwanza.

Aliongeza pamoja na serikali kuruhusu michezo irejee, lakini itaendelea kuchukua tahadhari katika maeneo yatakayohusisha michezo hiyo ili kujikinga na corona.

"Wachezaji wote watakaoshiriki michezo watapimwa joto kabla ya mechi kuanza, lakini pia mashabiki kwa kipindi hiki hawataingia uwanjani, tunaangalia uwezekano wa kuruhusu idadi fulani ya mashabiki kama vile vikundi vya ngoma ili uwanja usiwe kimya kabisa," aliongeza Mwakyembe.

Aliliagiza Baraza la Michezo Tanzania (BMT), kuanza kuweka taratibu mbalimbali kuhusiana na usimamizi wa michezo mingine ambayo itafanyika hapa nchini.

Alisema pia Kituo cha Televisheni ya Taifa (TBC), huenda kikaonyesha mechi za Ligi Daraja la Kwanza na Ligi Daraja la Pili katika kipindi hiki ambacho mashabiki hawaruhusiwi kuingia viwanjani.

## Simba, Yanga hakuna kulala

**Na Saada Akida**

VIGOGO wa soka nchini, Simba na Yanga zinatarajia kuwaita wachezaji wake ili kuanza mazoezi ya pamoja kwa ajili ya kumalizika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa mwaka 2019/ 20.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema jana timu yao itaanza mazoezi ya pamoja Juni Mosi, mwaka huu chini ya Kocha Msaidizi, Boniface Mkwassa na tayari wameshawajulisha wachezaji wao.

Bumbuli alisema klabu imeshaanza kuandaa utaratibu wa kuwarejesha wachezaji wao na makocha wao walikuwa nje ya nchi ili kuungana na wenzao mapema.

"Kwa upande wa makocha wetu wa kigeni wakiongozwa na Luc Eymael, hakuna hakika kama watarejea mapema, kwa sababu wenzetu bado viwanja vya ndege havijafunguliwa, hivyo timu itakuwa chini ya Mkwasa na makocha wengine waliokuwapo," alisema Bumbuli.

Alisema ili kujikinga na corona, daktari wa timu hiyo atafuata ushauri uliotolewa na Wizara ya Afya na mamlaka husika kuwapima wachezaji kabla ya kuanza kufanya mazoezi ya pamoja.

" Leo (jana) asubuhi wataalum wa viwanja wameanza kufanya ukarabati wa Uwanja wa Chuo cha Sheria, wanaweka alama za ndani ambazo zilifutika kutokana na kutotumika kwa muda mrefu ili tuweze kuutumia kama timu," Bumbuli alisema.

Naye Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kikosi chao kiko tayari kuendeleza kampeni yake ya kutetea taji hilo kama walivyofanya wakati msimu unaanza.

"Ni vitu vichache vya pamoja ndio vinasubiriwa, wote tuna hamu ya kumaliza msimu huu, tunataka kuwapa furaha mashabiki wetu, tunajua kiu yao," alisema Rweyemamu.

Simba ndio vinara na mabingwa watetezi wa ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >